BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**

9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii,**
			na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi,**

			Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**

29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Uwezeshaji,**	**-**	**Naibu Waziri wa Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg.	**Raya Issa Msellem**	**-**	**Katibu**

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 20 Juni, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika Kikao cha Baraza cha tarehe 7 Juni, 2018 Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi la Nam. 264. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aliahidi kujibu kwa maandishi, sasa namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mjumbe huyo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kama inavyokumbukwa kwamba mnamo tarehe 7 mwezi wa Juni, 2018 baada ya kujibu swali la msingi Nam. 264 lililouizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusiana na Hoteli ya Bwawani, Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf katika swali lake la nyongeza alitaka kujua idadi pamoja na majina ya Kampuni zilizoomba na kutarajia kushinda zabuni kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Hoteli ya Bwawani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kujitokeza kwa swali hilo la nyongeza niliahidi kujibu swali hilo la nyongeza kwa maandishi hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha na kuindeleza Hoteli ya Bwawani. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Mamlaka ya Vitega Uchumi ZIPA iliamua kutumia utaratibu wa kutoa mwaliko kwa maana ya *Restricted biddi ng* kama ulivyoelezwa katika Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2005 ambapo jumla ya wazabuni 5 walionekana kuwa na uwezo wa kuendeleza Hoteli ya Bwawani ili wawasilishe maombi yao. Wazabuni hao ni kama wafuatao:

1. *Index Group Limited*

2. *Victoria Real Estate Developers Co. Ltd*

3. *Nocturnal Inter Limited*

4. *Dhow Financial Limited*

5. *Quality Group Limited*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mwaliko huo wazabuni 2 waliweza kurejesha maombi yao nao ni:
Dhow Financial Limited na
Quality Group Limited

Wazabuni hao 2 walifanyiwa tathmini kwa ajili ya kumtafuta mzabuni 1 ili aweze kazi ya kuendeleza Hoteli hiyo ambapo Kampuni ya *Quality Group Limited* ilifanikiwa kuwa mshindi na kupatiwa mkataba kwa ajili ya kuendeleza Hoteli ya Bwawani. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu kwa shughuli inayofuata.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Waziri wa wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Hati Mezani Hotuba ya Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, Vile vile naomba kuwasilisha Hati Mezani Hotuba ya Kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi kwa Mwaka 2018/2019.

Mhe. Bahati Khamis Kombo (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Majumuisho ya Mijadala ya Bajeti ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Bahati Khamis Kombo kwa niaba ya Mwenyekiti sasa naomba nimwite tena Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kuwasilisha Hotuba na Maoni ya Kamati yake.

Hotuba ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Kuhusu Majumuisho ya Mjadala wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2018/2019

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti: *Bismilahrahmani Rahim* Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze sana nitangulize shukurani za awali kwa Mola wetu Mtukufu kwa kutuwezesha kudiriki siku ya leo katika hali uzima na afya njema. Aidha nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema ya pekee ya kuwa miongoni mwa waliokamilisha mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunamuomba atulipe malipo ya funga zetu zote na pia atuwasilishe tuone Ramadhani ya mwakani tukiwa wazima na kuitekeleza ibada hiyo kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tu napenda pia kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mhe. Spika na Naibu wake kwa namna ya pekee mnavyoliendesha Baraza hili ambalo limekuwa chachu kwetu na kuliona Baraza hili Tukufu likiwa katika hali njema zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Spika kwa hekima na busara zake nyingi ambazo analiendesha Baraza hili na nia moja inayonipa kuwa uongozi ni busara na uongozi ni *talent* Mhe. Spika, pamoja na umri wake mdogo amekuwa chachu ya kuendesha Baraza letu hili na tumshukuru sana. Lakini nimshukuru kwa aina yake ya kipekee kwa kuwa umri wake haufanani sana na busara zake, lakini vile vile nimshukuru Mhe. Naibu Spika, wa Baraza letu hili kwa namna ya pekee alivyoshirikiana nasi katika kuliendesha baraza hili lakini kushirikiana nasi katika Kamati hizi. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nikupongeze wewe pamoja na msaidizi wako au mwenyekiti mwenza Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa kazi kubwa mnayoifanya, lakini vile vile kwa aina ya kipekee sana niishukuru sana Kamati yangu na Wajumbe wake wote kwa kunipa ushirikiano mkubwa wakati wote wa kipindi cha Kamati yetu na hekima kubwa ambazo kamati yangu inazitegemea na kunishauria pale ambapo tunaweza tukapotoka kibinaadamu nawapongeza sana na ninawashukurua sana.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati zote kwa kunipa mashirikiano makubwa sana wakati nikijumuisha Hotuba yangu. Lakini vile vile niwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kipindi cha miaka 2 wakati nikipewa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti walinipa mashirikiano makubwa sana na niseme tu uvumilivu wao umenipa changamoto kubwa sana ya kufanya kazi yangu kwa bidii kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri sana wote wa Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa walikuwa wakpata changamoto nyingi kwenye kamati yangu lakini zilikuwa ni changamoto za kuweza kufanya kazi kwa bidii na kuwatendea haki wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa upeo kubwa nianze Hotuba yangu. Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza mantiki yangu lakini kwanza vile vile niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mpendae kwa kuendelea kuniamini na nishukuru Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini nikapeperusha bendera yao. Lakini kwa aina ya pekee niwashukuru familia yangu kwa kunivumilia wakati nikitekeleza majukumu yangu (*Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nianze Hotuba yangu kama nilivyojipangia.Mhe. Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba tokea tarehe 9/05/2018 Baraza la Wawakilishi limekuwa katika mjadala wa Bajeti ya mwaka 2018/2019 ambapo bajeti za Wizara zote 14 zimejadiliwa na kupitishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kuchukuwa fursa hii, kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kukamilisha kazi kwa umakini na ufanisi mkubwa, kutokana na namna walivyochambua na kuzijadili bajeti za Wizara na kutoa

maoni yao ambayo bila shaka yalilenga kuzifanya kazi za bajeti hizo ziwe bora zaidi na zenye kuleta tija inayostahili kwa maslahi ya wanachi na taifa kwa ujumla, ili dhamira na malengo ya nchi yetu yaweze kufikiwa kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi inaelekeza kwamba, Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kuhusiana na hoja mbali mbali zitakazojitokeza wakati wa mjadala wa Makadirio ya bajeti za Wizara zote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Kamati ya Bajeti imetimiza masharti ya Kanuni hiyo, kwa kufanya kikao cha majumuisho kwa muda wa siku mbili tarehe 18/06/2018 na 19 /06/2018, na kufanikiwa kupitisha hoja mbali mbali za kibajeti zilizoibuliwa na Wajumbe wakati wakichangia bajeti za Wizara pamoja na maoni ya Kamati za kisekta yaliyowasilishwa Barazani kupitia hutuba za Kamati zao.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa marikiano yao walionionesha katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Aidha, napenda kuwapongeza kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuchambua hoja mbali mbali za Wajumbe zilizotokana na mijadala ya bajeti, ambazo ndio msingi wa Hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuzipa nguvu shukurani zangu naomba kuwatambua kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo;-

1.	Mhe. Mohamed Said Mohamed	Mwenyekiti
2.	Mhe. Bahati Khamis Kombo	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe
4.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Mjumbe
5.	Mhe. Shehe Hamad Mattar	Mjumbe
6.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	Mjumbe
7.	Mhe. Asha Abdalla Mussa	Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kuwatambuwa kwa kuwashukuru Makatibu wa Kamati ya Bajeti ambao wamekuwa na msaada mkubwa kwa Kamati yangu, ambao ni:-

1. Ndg. Abdalla Ali Shauri
2. Ndg. Asha Said Mohamed
3. Ndg. Kassim Tafana Kassim

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifanya majumuisho ya Mjadala wa Bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa kushirikiana na Serikali, kwa kushauriana kuhusu hoja mbali mbali za kibajeti zilizojitokeza wakati wa mijadala ili kuangalia maeneo ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisho au kuwekewa mazingatio maalum katika utekelezaji wake. Lengo la kuongeza ufanisi wa Bajeti. Hivyo nitaiwasilisha taarifa hii ambayo ni matokeo ya mashauriano hayo baina ya Kamati ya bajeti na Serikali kwa Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, Kikamilifu kwa kazi ya majumuisho ya mijadala ya Bajeti, Kamati ilikaa na Mawaziri wa Wizara zote kuhusiana na hoja ambazo pia waliambatana na watendaji wakuu wa taasisi zao, ili kuweza kusaidia ufafanuzi wa hoja hizo zilizoibuliwa. Aidha, kwa kuzingatia nafasi ya Wizara ya Fedha katika mchakato mzima wa Bajeti, kikao hicho pia kilimjumuisha Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohammed, ambae tunampongeza sana kwa kazi kubwa ambayo ameiufanya. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amekuwa ni chachu katika Kamati yangu mara hii tulishirikiana kikamilifu na alitupa mashirikiano ya kudumu sana nakupongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na uendelee na tabia hiyo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile alifuatana na watendaji wake wakuu katika Wizara hiyo akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Khamis Mussa Omar pamoja na baadhi ya Watendaji wote tunawapongeza sana kwa mashirimiano makubwa. Kamati vile vile inapenda kuwashukuru Mawaziri pamoja na watendaji wote kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kukamilisha zoezi hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati kwa kuzingatia umuhimu wa Kamati za Kisekta katika majumuisho majumuisho hayo, Kamati pia iliwaalika Wenyeviti wa Kamati za Kudumu kwa lengo la kushauriana nao juu ya hoja na changamoto za kibajeti hususan katika sekta wanazozisimamia tunawapongeza sana waheshimiwa Wenyeviti. Kamati vile vile ya Bajeti inawashukuru Wenyeviti wa Kamati kwa ushrikiano wao waliotupatia katika kutoa maoni ambayo yamejenga katika kufanikisha majukumu ya Kamati kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, hoja zilizojitokeza katika mijadala hii ni nyingi sana kimsingi Kamati inazitambua zote kuwa ni muhimu. Hata hivyo, naomba ieleweke kuwa Hotuba hii imejumuisha baadhi tu ya hoja hizo kwa kuzingatia uhusianao wake na vifungu vya bajeti, ufafanuzi wa hoja hizo ulitolewa na Serikali wakati wa mjadala na matokeo ya mashauriano baina ya Kamati na Serikali kuhusu hoja hizo wakati wa kikao cha majumuisho ya bajeti.

MAENEO YALIYOCHANGIWA NA WAJUMBE WENGI

Mhe. Mwenyekiti, maeneo ambayo yaliyochangiwa na Wajumbe wengi na nitaeleza kama ifuatavyo:

1. Uimarishaji wa Maslahi ya Walimu pamoja na ajira za walimu wa kujitolea
2. Changamoto katika Utekelezaji wa Mfumo wa Ugatuzi
3. Changamoto za Miundombinu ya Barabara
4. Tatizo la kuongezeka kwa vitendo vya Udhalilishaji wa kijinsia

Mhe. Mwenyekiti, hii naomba niirejee

4. Tatizo la kuongezeka kwa vitendo vya Udhalilishaji wa kijinsia

5. Kusuasua kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi mikubwa ya Maendeleo
6. Umuhimu wa kutumia mifumo ya kisasa katika kukusanya mapato
7. Nidhamu katika Matumizi ya Fedha za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, na hii naomba niirejee.

7. Nidhamu katika Matumizi ya Fedha za Serikali
8. Changamoto za kuchelewa kwa ripoti za mwaka za ukaguzi za Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
9. Changamoto katika Utaratibu uliopo wa kukabiliana na maafa
10. Changamoto za Huduma katika sekta ya afya
11. Changamoto za upatikanaji wa huduma ya maji
12. Changamoto za Uendeshaji wa Meli ya M.V Mapinduzi II
13. Changamoto za Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ambalo hili linaongeza kuwa ni hoja moja ambayo tunasema tayari tunaingia kwenye kero za Muungano ambayo inaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nitowe tu hoja zile zilivyoelezwa lakini pamoja nayo niweze kueleza majibu ya Serikali lakini sambamba na hilo nitaeleza na maoni ya Kamati baada ya kuchambua na kukubaliana na hoja hizo, kimsingi hoja zote tumekubaliana nazo lakini kwa utaratibu nitaomba tu nizisome kama ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kwanza ni Tume ya Uchaguzi nitaanza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndii inayoongoza Baraza hili la Wawakilishi sasa nitaanza nayo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Hoja Zilizotokana na Mjadala wa Bajeti kwa Mwaka 2018/2019

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

TUME YA UCHAGUZI: Waheshimiwa Wajumbe walipendekeza Bajeti ya Tume ya Uchaguzi iongezwe kutokana na unyeti wa majukumu yake, ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilipangiwa Tsh bilioni 695,500,000 na mwaka wa fedha 2018/2019 imepangiwa Tsh. bilioni 1,774,100,000. Aidha, Majengo ya Tume ya Uchaguzi yako katika hali mbaya ikiwemo majengo ya ghorofa la Wilaya ya Kaskazini "A" ambapo miundombinu yake haiwawezeshi watu wenye ulemavu kulitumia kwa wepesi. Kwa Afisi za Wilaya ya Kaskazini "B" kuna changamoto ya ufinyu wa ofisi kiasi cha kushindwa kuhudumia watu watatu kwa wakati mmoja.

Mhe. Mwenyekiti hii ndio hoja ya 1 lakini hoja hii ilijibiwa na Serikali kama ifuatavyo:-

Wizara iliiarifu Kamati kuwa bajeti iliyopangwa ya Tsh. bilioni 1,774,100,000 inatosheleza katika kutekeleza majukumu ya kuhudumia Ofisi na pia wamekiri kuwa wamepata ongezeko la asilimia 5 ya fedha za bajeti ya 2018/2019, kulinganisha na Bajeti ya 2017/2018 na hivyo hakuna changamoto ya fedha. Aidha, kuhusiana na majengo ya Tume kuwa hali mbaya, Wizara imeeleza kamati kuwa imeomba maeneo kwa ajili ya

ujenzi wa ofisi mpya za Tume katika Wilaya ya Kaskazini A, Wilaya ya Kaskazini B, Wilaya ya Magharib A na Wilaya ya Magharibi B. Hivyo wameomba viwanja kupitia Wizara ya Ardhi na tunatarajia tu kipindi kifupi kijacho kuwa Wizara ya Ardhi itaona ombi hili ili iweze kuwapa kwa haraka sana.

MAONI YA KAMATI

Kamati ilikubaliana na kiwango ambacho Wizara imeridhia kupatiwa kwa kuwa imekiri fedha zilizotolewa inatosheleza katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili katika Wizara hii ilikuwa Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo (*CDF*) Wajumbe wengi walichagia kuhusiana na Fedha chache zinazotolewa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDF)* ambapo kwa sasa zinatolewa jumla ya Tsh. milioni 20 na imependekezwa ziongezwe Tsh milioni tano (5) ili ziwe milioni ishirini na tano (25).

Majibu ya Serikali:

Serikali imekiri kuwa fedha zinazotolewa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDF)* katika majimbo ni chache na imeahidi kulifanyia kazi suala hili kuhakikisha kuwa zinaongezeka kwa mujibu wa uchumi utakavyoimarika. Katika bajeti zijazo Serikali imekiri kuwa italifanyia kazi kwa wepesi zaidi ili kuona basi mfuko huu umeongezeka.

Maoni ya Kamati:

Wajumbe wamesisitiza juu ya kuongezwa kwa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDF)* kwa kuwa majimboni kuna shughuli nyingi ambazo zinatakiwa kutekelezwa na pia kufanyiwa uchambuzi wa kina kuhusiana na fedha hizo zilivyotumika za mfuko wa jimbo kama zililivyokuwa ni chachu ya maendeleo ya majimbo yetu.

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, napo vile vile palikuwa na hoja na hoja ya kwanza ilikuwa kama ifuatavyo:

IDARA YA URATIBU NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE YA NCHI

Kumekuwepo na changamoto ya baadhi ya wataalamu wa sekta mbali mbali, kushindwa kushiriki katika mikutano ya mashirikiano ya kikanda tokea hatua za awali kutokana na ufinyu wa fedha, licha ya baadhi Mawaziri kushiriki katika mikutano hiyo na kupelekea kushindwa kuiwakilisha Zanzibar ipasavyo. Kwa msingi huo, Wajumbe wamependekeza Idara hii kwa bajeti ya mwaka 2018/2019 itengewe fedha za kutosha na pia zipatikane kwa wakati ili utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusu Zanzibar ipatekane uwakilishi wa wataalamu tokea hatua za awali. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Idara hii imepangiwa bajeti ya Tsh 537,965,000.

Majibu ya Serikali:

Kamati imearifiwa kuwa, Bajeti imetengewa kwa Idara hii inatosheleza kwa mujibu wa watendaji wanaotarajiwa kusafiri kwa kuzingatia kuwa Idara hii kazi zake ni kuratibu tu. Aidha, fedha ziliyotengwa ni kwa ajili ya safari ya watendaji kama ilivyo kwa Wizara nyengine ambazo nazo kila moja ina bajeti yake kwa shughuli za kuhudhuria mikutano ya kikanda.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na ufafanuzi wa Wizara, na kwakuwa Wizara imekiri kuwa Bajeti hiyo inatolesheleza, Kamati imeridhia fungu hilo kubakia kama lilivyo.

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI
ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi walizungumzia kuhusiana na mradi wa *CCTV* Camera ambao kwa mwaka wa fedha 2018/2019 umetengewa Tsh bilioni 20. Wajumbe walishauri kati ya fedha hizo zipunguzwe shilingi bilioni 5 na zielekezwe kwenye kuimarisha barabara za ndani, mbazo bado zinauhitaji mkubwa wa fedha ukilinganisha na uwezo halisi wa kifedha uliopo hivi sasa. Aidha, kwa kipindi cha miaka mitatu Wizara imepokea shilingi bilioni 4,600,000,000/- tu kwa ajili ya uendelezaji wa barabara za ndani *(Feeder road).*

Majibu ya Serikali:

Kamati imearifiwa kuwa, Mradi huu ni wa miaka mitano na Serikali inalazimika kulipa kwa mujibu wa mkataba wa mradi huo. Kwa hivyo inashauriwa fedha hizo zisipunguzwe. Fedha kwa ajili ya barabara za ndani zinatokana na Mfuko wa Barabara. Ambapo katika mgao wa mfuko huo asilimia 15 zinapelekwa Halmashauri kwa ajili ya kuendeleza bararabara za nadani. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mtaa na Idara Maalum za SMZ, pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji zitakaa pamoja kuangalia namna ya kuongeza asilimia ya mgao wa mapato ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuimarisha barabara za ndani.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na maelezo ya Wizara na imekubali fedha za Mradi wa *CCTV* zibakie kama zilivyo. Aidha, Kamati inaunga mkono wazo la kuongeza mgao wa fedha za mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuimarisha barabara za ndani. Hivyo, Kamati ya Bajeti inaitaka Kamati ya Sekta kulifuatilia suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaomba sana kwa niaba ya Mhe. Spika, kamati ya kisekta kuanza kufuatilia na kamati ya Sheria na Katiba ndio yenye jukumu hili kwa

hivyo jukumu hili tunawapa kufuatilia kwa makini zaidi, ili baadae waje waliarifu Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili ilikuwa Wajumbe wengi hawakuridhishwa na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato katika masoko ikiwemo mapato ya maegesho *(parking)*, kulinganisha na huduma zinazopatikana pamoja na mazingira ya masoko hayo yalivyo, masoko hayapo katika hali nzuri.

Majibu ya Serikali:

Kamati imearifiwa kuwa mfumo wa ukusanyaji wa Mapato unatarajiwa kuwa kwa njia ya kielektroniki baada ya kipindi cha miezi miwili hadi mitatu. Aidha, Wizara imekiri kwamba miundombinu katika masoko hairidhishi kabisa. Hivyo, Wizara imeahidi kuwa itafanya maboresho baada ya kumalizika kwa kipindi cha mvua.

Maoni ya Kamati:

Kamati imependekeza wananchi wapatiwe elimu kuhusu maeneo yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa kwa ajili ya maegesho *"parking"*. Kamati pia imeshauri kuanzishwa maeneo ya maegesho ya ghorofa ambayo yanakwenda sambamba na ukuaji wa mji. Pia Kamati imependekeza utakapoanza mfumo wa elektroniki kuwepo na utaratibu wa ukaguzi wa malipo ya maegesho ili kudhibiti uvujaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ilikuja hasa kulingana na hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyotoa jinsi ya kupanga mambo ya *packing* mjini na jinsi ya *holiday* hizi kuzitumia kwa mambo mengi ya *packing*. Tunaiomba tu Serikali iweza kufuatilia jambo hili ili tuone umakini na ubora umepatikana katika kupanga *packing*, lakini vile vile kuona siku za *holiday packing* baadhi yao zinakaa *free* ili wananchi waweze kuona jinsi gani wanavyoweza kuzitumia kiurahisi zaidi.

OFISI YA RAIS KATIBA , SHERIA, UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora nayo ilikuwa na hoja kama zifuatavyo:

Katika bajeti ya mwaka 2018/19 Mahakama imepangiwa matumizi ya uendeshaji wa ofisi shilingi bilioni 1,515,100,000/= na Tsh. bilioni 1,113,800,000 za ruzuku. Wajumbe walishauri kuongezwa kwa fedha hizo kwa kuwa mara nyingi Mahkama imekuwa ikishindwa kuwawezesha mashahidi kuhudhuria mahkamani na kusababisha kusuasua kwa kesi.

Majibu ya Serikali:

Wizara imekiri kuwa bajeti iliyotengwa kwa mahkama kuu haitoshelezi katika kutekeleza majukumu yake. Fedha za matumizi mengineyo *(Other charges)* za kila mwezi

hazitoshelezi kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa mahkama. Hata hivyo, bajeti hiyo ni kwa mujibu wa ukomo *"ceiling"* uliowekewa. Hivyo, Mahkama inafanya kazi kwa mujibu wa vipaumbele vyake kulingana na fedha walizozipangia.

Maoni ya Kamati:

Kutokana na changamoto zilizopo katika Mahkama, Kamati inapendekeza Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na kuangalia namna ya kutatua changamoto zilizopo katika Mahkama ili kuleta utendaji ulio na ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka sana Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala Bora ulizungumzia uchakavu wa majengo mengi ya Mahakama yetu, kwa hivyo tungeomba tu Wizara hizi zikae pamoja ili kutatua changamoto ambazo zinaweza zikajitokeza kwa urahisi ili kupata ufanisi wa Mahakimu na Majaji wetu kufanya kazi sehemu zilizokuwa salama zaidi.

Mhe. Mwenyekiti hoja ya pili: Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeshauri Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi *(ZAECA)* kupitia bajeti ya mwaka 2018/2019, ipatiwe vyombo vya usafiri hususani Afisi za Pemba ambazo zinatumia gari moja tu kwa Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limekua likiathiri utendaji wao na kukosa ufanisi katika maeneo yao ya kazi.

Majibu ya Serikali:

Wizara imekiri ni kweli wana tatizo la usafiri ambalo linapunguza ufanisi wa shughuli za *ZAECA* Pemba. *ZAECA* wameshindwa kuweka mpango wa ununuzi wa gari kutokana na ukomo wa bajeti *"ceiling"* walioekewa. Kwakuwa taratatibu zinaruhusu, Wizara ya Fedha imewashauri *ZAECA*, ikiwa suala la gari ndio kipaumbele chao waombe kibali kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa ajili ya kununua gari kwa kuhaulisha fedha ndani ya vifungu vya bajeti yao.

Maoni ya Kamati: Kamati inapendekeza *ZAECA* wauchukue ushauri wa kuhaulisha vifungu vya bajeti ili waweze kununua gari. Pia Kamati imependekeza Wizara ya Fedha iangalie uwezekanao wa kuwapatia *ZAECA* gari miongoni mwa gari zilizo rejeshwa na Taasisi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti hoja ya Tatu katika Wizara hii: Kamati ya *PAC* haikuridhishwa na ucheleweshaji wa ripoti za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ambazo zipo nyuma sana, wakati tupo katika bajeti ya mwaka 2018/2019 ndio kwanza Ofisi hii imekamilisha ukaguzi wa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, Kamati ilisikitishwa kutoridhishwa kutoletwa Barazani Ripoti za Ukaguzi wa Miradi na Programu za Maendeleo kuwasilishwa kwa Wajumbe wa Baraza kupima ufanisi wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Kamati imearifiwa kuwa, kwa mujibu wa taratibu za ukaguzi ripoti hizo hazijachelewa kama inavyoelezwa kwakuwa ni lazima kwanza ifanyiwe matumizi kabla ya kufanywa ukaguzi na baada ya miezi mitatu ya matumizi ndio ukaguzi unapaswa kufanyika. Aidha, Serikali imekiri ni kweli kuna mashirika hayajawasilishi ripoti zao Barazani na kuahidi litalifanyia kazi suala hilo ili Mashirika hayo yawasilishe ripoti zao kwa mujibu wa Sheria.

Maoni ya Kamati: Kamati imeitaka Serikali ilifanyie kazi suala la ucheleweshwaji wa ripoti za *CAG* kwa kuyaainisha mashirika yote yanayopaswa kuleta ripoti zake Baraza la Wawakilishi na kuhakikisha ripoti hizo zinawasilishwa kama ulivyo utaratibu. Aidha, imependekezwa pia kuwe na uwazi katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *"CAG"* ili jamii ifahamu kinachoendelea.

WIZARA YA HABARI UTALII NA MAMBO YA KALE

Mhe. Mwenyekiti, hapa napo vile vile pana ripoti nyingi lakini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya TSh. 4,344,000,000/= ambazo zitaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia ilipangiwa kukusanya Sh. 3,113,600,000/= ambazo zitatumika na taasisi husika. Katika utekelezaji halisi, Wizara ilikusanya Sh. 2,924,572,780/= sawa na asilimia 61 zilizoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Lakini kwa upande wa makusanyo yanayobakia katika Taasisi, Wizara ilifanikiwa kukusanya Sh. 3,515,703,680/= sawa na asilimia 111 ya malengo kama ilivyoelezwa katika utekelezaji. Wajumbe walihoji juu ya makusanyo yanayobakishwa kwenye taasisi kuwa ni mengi zaidi na kuzorota kwa makusanyo yanayopelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Waheshimiwa hapa naomba nitanabahishe tu kitu gani ambacho Waheshimiwa Wajumbe walikisema sana, zile pesa ambazo Wizara ilipewa jukumu la kukusanya wenyewe kupeleka Mfuko mkuu wa Serikali, hazikufikia ile asilimia ambayo ilitakiwa ikusanywe. Lakini zile ambao zilitakiwa kukusanywa kwa matumizi yao wenyewe zilivuka lengo. Sasa hapa walitaka kujua kwa nini wao pesa ambazo ilikuwepo zilivuka lengo, lakini zile ambazo walitakiwa wazikusanywe wazitumie wao ndio zilivuka lengo, hapa ndipo palipokuwa na utata mkubwa.

Majibu ya Serikali:

Wizara imekiri ni kweli haikuvuka malengo ya makusanyo yaliyoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kutokana na kuwekewa malengo makubwa ya makusanyo kwa bajeti ya mwaka 2017/2018 kulingana na uwezo wao wa kukusanya. Aidha, Kutokana na historia yao ya nyuma ya ukusanyaji mapato, shabaha waliyowekewa mwaka huu pia ni kubwa sana. Hivyo, kiuhalisia kiwango hicho walichokusanya sio kidogo kulinganisha na uwezo wa Wizara.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara. Aidha, Kamati imependekeza Wajumbe wapatiwe mafunzo kuhusu masuala ya bajeti ili dhana ya ubakizaji mapato *(retention)* kwa tasisi zinazokusanya mapato ili ieleweke uhalisia zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ya pili: Kamati ya Maendeleo, Wanawake, Habari na Utalii, haikuridhishwa na uendeshaji wa *ZBC 2* kupitia mkataba uliofungwa baina ya Shirika la Utangazaji la *ZBC* na Kampuni ya *Azam Media LTD* kwa ajili ya uendeshaji wa *channel ZBC 2* hivyo, kutokana na kutoonekana mapato yanayotokana na matangazo ya *ZBC 2* kupitia mkataba huo kamati yenyewe ya kisekta haikuridhika na jambo hili.

Majibu ya Serikali:

Wizara imekiri ni kweli hakukuwa na mapato yanayotokana kupitia Mkataba huo, ingawaje Mkataba huo ulikuwa umejikita zaidi katika suala la mashirikiano, kwa kuandaa na kurusha vipindi vya pamoja na kugawana mapato. Aidha, Wizara imeiarifu Kamati kuwa mkataba wa awali umemalizika tokea tarehe 15/03/2018, na kwa sasa wapo kwenye utaratibu wa kujadiliana kuhusu mkataba mpya. Wizara imeomba ipewe muda ili kuhakikisha kasoro zilizojitokeza awali hazijirejei tena katika mkataba mpya unaotegemea kuandaliwa.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeishauri *ZBC* na Serikali kwa ujumla kuwa makini katika kusimamia mikataba ili kuhakikisha ufanisi wa mikataba hususan katika masuala ya mapato. Aidha, Kamati imeagiza kupatiwa kivuli cha Mkataba huo wa makubaliano baina ya *ZBC na Azam Media LTD* ili ijiridhishe mkataba huo kweli ulikuwa hauna mapato au la. Vile vile kamati inaishauri taasisi husika au kamati husika ya kisekta iweze kulifuatilia suala hili kwa umakini zaidi.

Hoja ya tatu Mhe. Mwenyekiti: Wajumbe wengi walichangia kuhusu umuhimu wa kuitangaza zaidi Zanzibar Kiutalii hasa ikizingatiwa kwamba ni moja kati ya maeneo ya vipaumbele vya nchi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii imetengewa Tsh milioni 533,145,000 tu. Aidha, Wajumbe walichangia kuhusu kuimarisha maeneo ya kihistoria na vivutio vya ndani ambavyo iwapo vitaimarishwa mapato ya sekta hii yataongezeka mara dufu.

Majibu ya Serikali:

Wizara imekiri, ni kweli bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kuutangaza Utalii ni ndogo, hata hivyo, kutokana na ukomo wa bajeti *"ceiling"* na uwezo wa Serikali kiwango hicho kinatosha kutekeleza majukumu waliyojiwekea. Aidha, Wizara imesisitiza kulingana na fedha wanayopatiwa utendaji wao ni mkubwa hasa ikizingatiwa kiwango cha watalii wanaoingia nchini kinaridhisha kulinganisha na bajeti wanayotengewa kwa ajili ya kuutangaza Utalii.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara na kuipongeza kutokana na kazi kubwa wanayoifanya. Hata hivyo Kamati, imesisitiza Wizara kuitangaza zaidi Zanzibar kupitia balozi zilizopo nje ya nchi pamoja na kuweka taarifa muhimu zinazohusiana na Zanzibar ambazo zimekosekana katika balozi zetu. Kamati vile vile imeshauri Wizara ifanye utafiti katika visiwa vilivyopo Zanzibar ili zijulikane rasilimali zilizopo ambazo zinaweza kusaidia na kuwa na mchango mkubwa katika kuwavutia watalii.

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, WANAWAKE NA WATOTO

Wajumbe wengi walijenga hofu na kuomba ufafanuzi kuhusu fedha za Programu ya Kukuza Maendeleo ya Wanawake na Kupinga Udhalilishaji ambayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imetengewa Tsh. bilioni 1.7 kwakuwa inaonekana fedha hizo zimeongezeka maradufu kulingana na fedha za mwaka 2017/18, licha ya ukweli kwamba vitendo vya udhalilishaji bado vinaendelea kuongezeka.

Majibu ya Serikali:

Kamati imearifiwa kuwa sababu ya Bajeti ya Fungu la Programu ya Kukuza Maendeleo ya Wanawake na Kupinga Udhalilishaji kuwa kubwa ni kutokana na mikakati iliyowekwa ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji, ikiwa ni pamoja na kulipia malipo ya waratibu wa vitendo vya udhalilishaji. Aidha, fungu hili linaonekana kubwa kutokana na kuunganishwa Programu ndogo mbili, yaani Programu ya Uratibu wa Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake na Programu ya Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Kuhusu hoja ya kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji, Wizara imeeleza kuwa vitendo vya udhalilishaji havijaongezeka isipokuwa kwa sasa wananchi wamehamasika kuripoti matukio ya vitendo hivyo katika Mamlaka husika.

Maoni ya Kamati: Kamati imependekeza kwa bajeti ya mwaka 2019/2020 Wizara itoe ufafanuzi zaidi kwa programu ambazo zimefanyiwa mabadiliko makubwa ya fedha kupitia kitabu cha Hotuba cha Mhe. Waziri ili Wajumbe wajuwe matumizi halisi ya fedha hizo badala ya kuzichanganya.

Hoja ya Pili

Kuhusu Kutofautiana Malengo kwa Utoaji wa Mikopo, Wajumbe walihoji kuhusu kutofautiana kwa malengo ya utoaji wa Mikopo kwa mwaka 2018/2019 baina ya Kitabu cha Hotuba ya Mhe. Waziri na Kitabu kikubwa cha Bajeti ambacho Wajumbe waliidhinisha, katika Kitabu cha Hotuba ya Mhe. Waziri imeelezwa kuwa Wizara inatarajia kutoa Mikopo 600 lakini kwenye Kitabu kikubwa Wizara inaonekana kupanga kutoa Mikopo 500. Aidha kwenye utekelezaji wa mwaka 2017/2018 pia kuna tofauti ya Idadi ya Mikopo iliyotolewa baina ya Kitabu cha Hotuba na Kitabu kikubwa. Kwenye Kitabu cha Hotuba imeripotiwa kuwa Wizara ilitoa jumla ya Mikopo 279 lakini kwenye Kitabu kikubwa imeripotiwa kuwa Wizara imetoa mikopo 300.

Wizara imeeleza kuwa tofauti ya Malengo ya Idadi ya Mikopo iliyotolewa kwa mwaka 2018/2019 inatokana na makosa ya kiuchapaji. Aidha, kuhusiana na tofauti ya Idadi ya Mikopo iliyotolewa kwa mwaka 2017/2018 inatokana na kutofikiwa Utekelazaji wa malengo ya mikopo hiyo.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhia ufafanuzi uliotolewa na Wizara juu ya utafauti wa taarifa baina ya vitabu viwili vya bajeti. Aidha, Kamati imeasisitiza kuwepo kwa umakini zaidi wakati wa kuandaa vitabu ili kuepuka makosa kama hayo yasijirejee tena.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo inayoongoza kwa hoja nyingi za Waheshimiwa Wajumbe, sijui kwa umakini wake au kwa sababu ipo karibu na wananchi.

Hoja ya Mwanzo:

Kutokana na changamoto nyingi katika sekta ya elimu ikiwemo ukosefu wa vifaa, ubovu wa madarasa, uhaba wa walimu, uchache wa vitabu vya kusomea na vikalio, Kamati ya Ustawi Jamii imependekeza fedha za bajeti ya Programu ya Elimu ya Sekondari TZS bilioni 95.6 zilizotengwa kwa mwaka 2018/2019, zipatikane kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Programu hii ilitengewa Tsh 63.5 bilioni, hadi kufikia machi 2018 jumla ya Tsh 27.4 bilioni tu ndizo zilizopatikana sawa na asilimia 43 kiuhalisia.

Majibu ya Serikali:

Fedha zilizochelewa kupatikana ni fedha za wahisani tu, kwa upande wa fedha za SMZ za Maendeleo pamoja na fedha za matumizi ya kawaida zote zimepatikana kwa wakati na kwa kiwango kizuri. Aidha, changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika sekta ya elimu zinaendelea kufanyiwa kazi.

Kamati imekubaliana na hoja hiyo bila ya marekebisho yoyote.

Hoja ya Pili:

Kamati ya Ustawi wa Jamii imearifu kuwepo kwa madeni ya walimu yanayotokana na malimbikizo ya stahiki za mishahara kama vile posho za likizo, masawazisho ya stahiki baada ya kumaliza masomo ya juu (mishahara) na posho za likizo, masawazisho ya stahiki baada ya kumaliza masomo ya juu ya mishahara yao na posho za nauli. Kutokana na changamoto hiyo ambayo ni ya muda mrefu. Kamati imetoa wito kwa Wizara kuchukua hatua za kusawazisha malimbikizo hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa walimu.

Majibu ya Serikali:

Wizara imearifu kwamba madeni yote ya malimbikizo ya walimu pamoja na wastaafu yameshalipwa hadi kufikia mwaka 2016.

Maoni ya Kamati:

Kamati inashauri Wizara kuendelea kulifuatilia zaidi suala la malipo ya madeni ya walimu ili kuwaondoshea usumbufu. Kamati inasisitiza suala hilo kwakuwa bado kuna malamiko kwa baadhi ya walimu kuhusu madeni hayo. Aidha, iweke utaratibu mzuri ambao hautowapa usumbufu waalimu katika kufuatilia stahiki zao.

Hoja ya Tatu:

Wajumbe wengi wameonesha kutoridhishwa na maendeleo ya Ujenzi wa vituo vya elimu Amali vya Daya-Mtambwe na Makunduchi. Kwakuwa kuna ongezeko la fedha kwenye Programu ya Elimu Mbadala na Mafuzno ya Amali, ambapo kwa mwaka 2017/2018 Programu hii ilitengewa Tsh bilioni 17.1 na kwa mwaka 2018/2019 imetengewa Tsh bilioni 24.5. Wajumbe wameitaka Wizara kuhakikisha changamoto hii inatatuliwa ndani ya mwaka huu wa fedha, kwa kuhakikisha majengo hayo yanendelezwa na kufikia hatua ya kuridhisha.

Majibu ya Serikali:

Wizara imekiri kuwepo kwa matatizo yanayohusiana na mkandarasi katika mkataba wa mwanzo ambao umekwisha muda wake na kwasasa wamesaini mkataba mpya kwa ajili ya utekelezaji kazi. Aidha, Wizara imeahidi kufanya jitihada ili changamoto hizo kwa mkandarasi wa awali aliyejitokeza tena.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeishauri Wizara kuendelea kusimamia kwa ukaribu ujenzi wa vituo vya Elimu ya Amali na pia kuanzisha kitengo cha majenzi katika Wizara ili kitakacho saidia kutatua baadhi ya changamoto hizo kuliko kuzikusanya pale kwenye Sera na Mipango ambapo inaonekana ipo nyingi sana.

Hoja ya Nne:

Kamati haikuridhishwa na fedha zilizotengwa katika Programu ya Ubora wa Elimu, ambapo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imetengewa Tsh. bilioni 7.7 tu, licha ya kuwa Programu hii inahusiana taasisi nyingi kama vile Taasisi ya Elimu Zanzibar, Baraza la Mitihani, Mrajis wa Elimu, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Shirika la Huduma za Maktaba, elimu mjumuisho, Vituo vya Mafunzo ya Walimu, *TEHAMA* pamoja na michezo.

Jibu la Serikali:

Wizara imeiarifu Kamati kuwa bajeti iliyotengwa ambayo ilionekana kuwa ni ndogo ni fedha za ruzuku kutoka Serikalini lakini pia kuna fedha nyengine za miradi zinazochangiwa na washirika wa maendeleo.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na majibu ya Wizara na kupitisha hoja hii bila ya mabadiliko yoyote.

WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

Hoja ya Kwanza:

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo haikuridhishwa na bajeti ndogo iliyotengwa kwenye Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda (SR010201), ambayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imetengewa jumla ya shilingi 3,665,290,000. Kiwango hicho kinaonekana ni kikubwa kikilinganishwa na fedha zilizotengwa mwaka 2017/2018 ambazo ni shilingi 644,987,000. Lakini kiuhalisia fedha hizo hazitoshi hata kuanzisha kiwanda kimoja na kwa msingi huo imependekezwa programu ndogo hiyo iongezwe fedha zaidi kwa nia ya kuanzisha viwanda na kuvifanya na kuwa endelevu.

Majibu ya Serikali:

Wizara imekiri kuwa fedha zilizotengwa kwa Programu ndogo ya ukuzaji viwanda (SR010201) ni ndogo na hivyo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/2019 imejipangia kuimarisha Taasisi ya SMIDA ambayo imeanza kazi zake rasmi mnamo tarehe 1 Julai 2018. Aidha pia Wizara imeimarisha maeneo tengefu ya viwanda kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo ambao watazalisha bidhaa zitakazokuwa na viwango stahiki.

Maoni ya Kamati:

Wajumbe wameridhia na majibu ya Wizara na hakukuwa na mabadiliko yeyote. Aidha, Kamati imeshauri serikali kuwa na mkakati wa kuendeleza maeneo tengefu yaliyotengwa pamoja na maeneo ya uwekezaji ya Micheweni, Amani na Fumba.

Hoja ya Pili:

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeshauri kusitishwa kwa mkataba baina ya Kampuni ya Jabal Kilimanjaro ya Dubai na Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*) inayohusiana na huduma ya ukaguzi wa magari yanayotokana na kuingizwa nchini kutoka Dubai. Mkataba huo umeelezwa kuwa asilimia 70 ya mapato ya shughuli hiyo yanaingia kwa Kampuni hiyo na asilimia 30 tu ndio inarudi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kamati imependekeza kusitishwa kwa Mkataba huo kwakuwa Kiwango kinachoingia nchini ni kidogo sana.

Majibu ya Serikali

Wizara imekiri juu ya kuwepo kwa matatizo katika mkataba uliofungwa baina ya Kampuni ya Jabal Kilimanjaro ya Dubai na Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*) na kuomba kuwa mkataba huo usivunjwe kwasasa, kwa kuwa unatarajiwa kumaliza muda mnamo 2020 na Wizara imeahidi kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Maoni ya Kamati:

Hoja imekubaliwa na wajumbe wa Kamati na pia kuomba kupatiwa nakala ya mkataba uliofungwa kwa lengo la kujiridhisha. Aidha, Kamati imesisitiza umuhimu wa kushirikishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kufunga mikataba ili kuepukana na mikataba isiyo na manufaa kwa serikali yetu. Mhe. Mwanasheria Mkuu Kamati yangu inakuomba ushughulikie vizuri sana mikataba hii ili kuona manufaa ya wananchi yamepatikana ipasavyo.

WIZARA YA VIJANA UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO

Maoni ya Kamati

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, haikuridhishwa na bajeti inayotengwa katika kuendeleza michezo hapa nchini. Kwa msingi huo Kamati imeomba serikali kuongeza bajeti ya Michezo, ili kuondokana na tabia ya kuomba omba hasa pale timu zetu zinaposhiriki mashindano ya Kimataifa. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Programu Ndogo ya Ukuzaji na uendelezaji wa Michezo imetengewa Tsh 368,400,000/-.

Majibu ya Serikali:

Wizara imeiarifu Kamati kuwa imejipanga vyema kwa bajeti ya Michezo na hivyo kwa mwaka huu wa fedha timu ya taifa itahudumiwa vizuri na kasoro zilizojitokeza katika kipindi cha nyuma zitarekebishwa.

Maoni ya Kamati:

Kwa kuwa Idara ya Michezo imetenga bajeti ya milioni 290 kwa ajili ya Timu ya Taifa, Kamati inasisitiza fedha hizo zitumike kama zilivyokusudiwa kwa ajili ya kuleta ufanisi katika sekta ya michezo na hivyo Kamati imeridhia hoja hiyo moja kwa moja.

Hoja ya Pili:

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii haikuridhishwa na kiwango cha bajeti kilichotengwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana kulingana na idadi ya Mabaraza ya Vijana yaliopo nchini ambapo kwa mwaka huu wa Fedha 2018/19 Programu ya Maendeleo ya Vijana imepangiwa milioni 457,448,000 pekee. Kamati imeshauri Bajeti hii iongezwe kwa kiwango kikubwa zaidi katika miaka ya usoni ili Idara iweze kuendesha mabaraza mengi zaidi pamoja ya miradi ya maendeleo iliyoanzishwa kupitia

Mabaraza hayo pamoja na kuwezesha kutatua changamoto zao zikiwemo kukosa ofisi na kupata sehemu ya kufanyia vikao.

Majibu ya Serikali:
Wizara imeiarifu Kamati kuwa katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 fedha walizopatiwa Baraza la Vijana zimefikia asilimia 70, ambapo miongoni mwa majukumu ya Baraza la Vijana ni kuratibu shuguli za vijana ikiwa ni pamoja na kutatua matatizo ya vijana ikiwemo ukosefu wa ajira, hivyo Bajeti hiyo inatosha kwa shughuli zilizopangwa.

Maoni ya Kamati

Hoja imekubaliwa na Kamati bila ya marekebisho yoyote, kutokana na maelezo mazuri, makubwa ambayo Wizara imejielekeza.

WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi wamehoji kuhusu ubora wa barabara zinazojengwa kutokana na kuharibika mara kwa mara hususan kipindi cha mvua, ambapo ukarabati unaofanywa kila zinapoharibika unaigharimu serikali fedha nyingi. Aidha, Wajumbe wamelalamikia kuchelewa kulipiwa fidia kwa baadhi ya barabara licha ya agizo la Mhe. Rais la kutaka barabara zote zilipiwe fidia.

Majibu ya Serikali:

Wizara imeieleza Kamati kuwa kuharibika kwa barabara kunatokana na matumizi mabaya ya barabara hizo ikiwemo kuongezeka kwa magari yenye uzito mkubwa kulinganisha na uwezo wa barabara na pia barabara zinazoharibika nyingi zao zilijengwa zamani. Aidha, Wizara imejipanga kuunda Kamati Maalum ambayo itashughulikia usimamizi wa ujenzi wa Barabara. Kuhusiana na Fidia Wizara imejitahidi katika kulipa fedha hizo na kumalizia madeni katika mwaka huu wa fedha.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaisisitiza Wizara juu ya kusimamia ujenzi wa barabara bora na imara. Aidha, Kamati imeshauri Wizara kuwa makini katika kuingia mikataba na kamapuni zinazojenga barabara hizo kwa kuhakikisha kuwa zinajengwa katika kiwango stahiki.

Hoja ya Pili:

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano imependekeza kuharakikisha kuifanya Karakana ya magari kuwa mamlaka ili iweze kuwa na maamuzi na kuimarisha utendaji kazi wake, hatua ambayo itaipunguzia serikali gharama kutokana na hali iliyopo sasa ambapo magari mengi hupelekwa gereji za watu binafsi kutokana na ukosefu wa vifaa vya kutosha katika karakana ya serikali.

Majibu ya Serikali:

Wizara kwa hatua ya awali imeelekzwa na serikali kuwa Karakana zote za Mawizara zitaunganishwa na kuwa chini ya Karakana kuu. Aidha, kwa sasa serikali imeagiza kuwa gari zote za serikali zinatakiwa kufanyiwa matengenezo katika karakana ya serikali baada ya kupelekwa kwenye karakana za watu binafsi.

Maoni ya Kamati:

Kamati inashauri kuwepo na mkakati mzuri wa kusimamia malipo ya gari za serikali zinazopelekwa karakana kwa ajili ya matengenezo ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za serikali.

WIZARA YA AFYA

Kamati ya Ustawi wa Jamii haikuridhishwa na bajeti iliyopangiwa Programu ya Kinga na Elimu ya Afya ambayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imetengewa Tsh bilioni 19,669,126,000/- sawa na asilimia 19.4 ya bajeti ya Wizara. Hivyo, Kamati imependekeza kwa mwaka ujao wa fedha bajeti ya Programu hii iongezwe ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kutekelezwa kwa ufanisi.

Majibu ya Serikali:

Wizara imeihakikishia Kamati kuwa fedha zilizotengwa kwa Programu ya Kinga na Elimu ya Afya inatosheleza katika kutekeleza majukumu ya programu hiyo. Aidha, programu ya Huduma ya Afya ya Msingi ambayo ilikuwa katika programu hiyo imegatuliwa katika Halmashauri na kwa msingi huo fedha zilizopo zinatosheleza.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhia na ufafanuzi wa majibu hayo bila ya pingamizi yoyote.

Hoja ya Pili:

Pamoja na juhudi zilizochukuliwa na serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya hasa katika ununuzi wa dawa, bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali na vituo vya Afya. Kutokana na changamoto hiyo, Wajumbe wengi walihoji juu ya usimamizi na utaratibu mzima unaotumika katika usambazaji wa dawa kutoka Bohari Kuu kwenda katika Vituo vya Afya.

Majibu ya Serikali

Wizara imeeleza kuwa Utaratibu uliokuwepo sasa ni kwamba dawa zinapelekwa katika kila Kituo cha Afya kwa mujibu wa maombi yanayopelekwa Bohari ya madawa kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo. Utaratibu huo unatumika kwa vituo vyote na Hospitali kubwa kama ya Mnazi Mmoja ambayo kwa kawaida huwa inaagiza dawa mara moja au zaidi ya mara 15 kwa mwezi. Aidha, kwa sasa bohari inatumia mfumo wa *M-system* ili

kufahamu dawa zilizotoka, kiwango chake na hospitali iliyopokea dawa hizo. Lakini pia kunatumika Mfumo wa *Electronic Logistic Management Information System (ELMIS)* kuagiza madawa bohari. Hivyo, kuna dawa za kutosha katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na japo kuna changamoto ndogo ndogo, kwa sasa serikali imefikia zaidi ya asilimia 80 ya upatikanaji wa dawa katika mahospitali japokuwa kuna changamoto ndogo ndogo zinazoendelea kujitokeza lakini wameahidi kuzifanyia kazi.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara na pia inaitaka Kamati husika ya Kisekta kufuatilia kwa karibu suala hili.

Hoja ya Tatu:

Kamati ya Ustawi wa Jamii imeishauri serikali kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Binguni kutokana na ukweli kuwa kwa bajeti iliyotengwa mwaka huu wa fedha hazitotosha kuanzisha ujenzi mkubwa wa hospitali hiyo ambayo inatarajiwa kuwa ya kisasa na yenye vifaa vingi vya gharama kubwa.Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 umepangiwa bajeti ya Tsh 14,000,000,000/-.

Majibu ya Serikali:

Fedha zilizotengwa kwa mradi wa ujenzi wa hospitali hii ni Tsh bilioni 4, lakini pia kumetengwa jumla ya Tsh. bilioni 15 kutoka kwa washirika wa maendeleo, hivyo ni imani ya wizara kuwa fedha hizo zitatosha kwa awamu ya mwamzo *"phase one"* ya mradi huo. Aidha Kamati Maalum imeundwa ili kuhakikisha mradi huo unakwenda vizuri katika utekelezaji wake.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na ufafanuzi uliotolewa na Wizara na kuagiza Kamati ya kisekta kuwafatilia kwa karibu zaidi.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe walihoji juu ya gharama kubwa wanayoibeba wananchi wakati wa kuunganishiwa huduma za umeme. Pamoja na utaratibu unaotumika wa kuunganishwa huduma hiyo kwa mkopo kwa wale wasiokuwa na uwezo wa kulipia gharama hizo papo kwa papo, ambapo wamelalamikia utaratibu huo kuwa hauwapi wananchi unafuu katika kupata huduma hiyo.

Majibu ya Serikali:

Kamati imeelezwa kuwa gharama inazoingia wananchi ni gharama za mwisho za kuunganishwa (*Point of end user*) hatua ambayo Shirika limefikisha miundombinu ya umeme kuelekea eneo ambalo wananchi wanahitaji kutumia huduma hii.

Hivyo, kwa wananchi ambao wanahitaji huduma kutoka (*Point of end user*), hulazimika kuchangia gharama za kuufikisha umeme huo sehemu anayohitajika. Lakini kwa kuzingatia hali za wananchi kunakuwepo na punguzo la gharama hizo. Shirika pia lina utaratibu wa kuwaunganishia wananchi na huduma ya umeme kwa mkopo usiokuwa na riba kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo.

Kamati imeshauri kuwa mkakati wa kusambaza umeme vijijini usiwe umeelekea eneo moja tu bali uzingatie mikoa na maeneo yote kwa ufanisi zaidi. Aidha Kamati ilisisitiza kuwa Shirika liendelee kutoa unafuu wa huduma za umeme hususan kwa kaya maskini ambazo mara nyingi inakuwa ni vigumu kuunganishwa umeme.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili, Wajumbe wengi walihoji juu ya kadhia inayowakabili watendaji wa Mamlaka ya Maji ZAWA kulipwa mishahara ya kima cha chini ambayo ni chini ya Tsh. 300,000 kinyume na agizo la Serikali kutokana na ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambalo lilielekeza kuanza kulipa mishahara ya 300,000 kwa watendaji wa kima cha chini. Aidha, Wajumbe walihoji juu ya kadhia ya upatikanaji wa maji licha ya kuwa kumekuwa na miradi mingi ya maji na fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha huduma hiyo.

Majibu ya Serikali:

Mamlaka imeeleza Kamati kuwa imeshindwa kulipa mishahara wa kima cha chini cha Shilingi 300,000 kutokana na kutoongezewa ruzuku yake ya 2.2 bilioni kwa mwaka 2017/2018. Aidha, pamoja na kuwaandikia Kamisheni ya Utumishi wa Umma mara tatu bado hawajapatiwa muungozo wa kulipa mishahara hiyo. Kwakuwa kwa mwaka 2018/2019 ruzuku ya Mamlaka iliongezwa wanategemea kuweza kulipa mishahara hiyo, baada ya kupata Muongozo kutoka Kamisheni ya Utumishi wa Umma pamoja na Idhini ya Bodi ya Shirika. Kuhusu malimbikizo ya mishahara ya ZAWA kwa mwaka 2017/2018

ZAWA kwa kuwa wanapokea karibia 80 asilimia ya fedha zake kutoka Serikalini, hivyo kwa sasa hawataoweza kulipa malimbikizo ya wafanyakazi kwa mwaka 2017/2018

Kuhusu changamoto ya maji, Mamlaka imeelezea kuwa miradi mingi ipo katika hatua nzuri isipokua miundombinu ya maji mingi ni chakuvu na hivyo kupelekea ubovu mkubwa katika miradi hiyo.

Maoni ya Kamati:

Kamati imemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ifuatilie suala la mishahara ya kima cha chini kwa mujibu wa agizo la Serikali katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Aidha kuhusu changamoto ya maji Kamati imemuagiza Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta afuatilie miradi ya ZAWA ambayo haijakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, tumuombe na Wizara, Waziri wa Nchi, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma nae afuatilie suala hili kwa karibu ili kuona basi wafanyakazi hawa wamepatiwa fedha zao kikamilifu.

WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UTALII

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi walichangia juu ya kilimo cha mwani ambacho kimeajiri wanachi wengi katika maeneo ya pwani, licha ya kukabiliwa na changamoto za bei ambapo haiendani na uhalisia wa ugumu wa kilimo chenyewe.Wajumbe walihitaji kufahamu Serikali ina mipango gani ya kuimarisha zao hilo ili kuwanufaisha wananchi waliojiajiri katika sekta hiyo.

Majibu ya Serikali:

Wizara imeiarifu Kamati kuwa, imeshajihisha wakulima wa mwani kujishahisha zaidi na kilimo cha mwani mnene katika kina kirefu cha bahari ambao una bei kubwa zaidi badala ya kulima mwani mwembamba ambao una bei ndogo katika soko la dunia. Aidha, Wizara imeshajihisha wawekezaji kuekeza viwanda vya kusarifu mwani kwa matumizi mbali mbali na pia inatoa taaluma kwa wananchi kufanya matumizi tofauti ya bidhaa zinazotokana na mwani ili kuongeza matumizi ya ndani ya nchi badala ya kusafirisha mali ghafi nje ya nchi.

Maoni ya Kamati:

Katika kuwahamasisha wananchi kwa kusarifu zao la mwani, Wizara iwawezeshe kwa kuwapatia taaluma pamoja na vifaa vya kuweza kusarifu. Aidha, Wizara itafute wakulima wa mwani soko la uhakika ili waweze kuhamasisha katika kuendeleza kilimo hicho.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kuwepo mahitaji makubwa ya matengenezo ya barabara, fedha zilizotengwa kwa bajeti ya 2017/2018 kupitia Mfuko wa Barabara zilitumika kwa kiwango kidogo sana (asilimia 26). Changamoto kama hiyo pia imejitokeza katika Utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha mambo ya Kale ambapo marekebisho ya Makumbusho ya Bihole na Makumbusho ya Dunga hayakufanyika kutokana na kutokamilika kwa utaratibu wa manunuzi (*procurement).* Changamoto hizi za manunuzi hazileti taswira nzuri katika utekelezaji wa bajeti na pia zinaweza kuathiri mipango ya maendeleo yanayopangwa kwa kuchelewa kutekeleza kwa wakati miradi inayopangwa.

Majibu ya Serikali:

Kuhusu changamoto iliyojitokeza ya fedha za Mfuko wa Barabara kutotumika Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji watakaa pamoja kuzitatua changamoto zilizojitokeza za Mfuko wa Barabara kwa lengo la kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha hizo.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na ufafanuzi uliotolewa na Wizara imeitaka Serikali kuhakikisha kuwa changamoto hii inapatiwa ufumbuzi wa karibu zaidi.

Hoja ya Pili, Wajumbe walitaka kupatiwa ufafanuzi juu ya fedha za mauzo ya zao la karafuu kwa mwaka 2017/2018 yaliyofikia jumla ya Tsh. bilioni 118.7 kwa tani 8,508.45 ambazo kimsingi zimekua hazionekani katika mzunguko wa fedha katika mabenki hususan kwa upande wa Pemba.

Wizara imeeleza kuwa itaiomba Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kufanya utafiti unaolenga na kufaham mzunguko wa fedha za mauzo za karafuu unavyokwenda.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na majibu ya hoja. Aidha, imependekeza suala la kufanyiwa malipo ya mauzo ya karafuu kwa njia ya benki ziangaliwe kwa makini zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, hizo ndizo hoja za msingi ambazo Kamati yangu imezipokea na kuzisanya wakati wote wa mjadala wa hoja ingawaje nimetoa hoja ambazo zile zilizokuwa na umuhimu mkubwa sana kibajeti na sikutoa hoja nyingi ambazo zipo, utakumbuka hoja thalathini na nne sasa ndio nimezisoma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusoma hutuba hii, baada ya majumuisho haya niwapongeze wajumbe wako kwa umakini mkubwa na kusiskiliza hoja hizi zilizotolewa na sasa naomba niwasilishe. (*makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ahsante nakushukuru Mhe. Mohammed Said (Dimwa), Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza naomba tutambue wageni wetu wa leo nao ni wageni wa Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa Mgogoni na Mwenyekiti wa Baraza, wageni wenyewe ni kama wafuatao:-

1. Ndg. Mzee Abdalla Ayoub ambae amefuatana na mwanawe Ndg Ali Abdalla Ayoub wote wanatoka Wingwi Mtakuja, lakini pia Mzee Abdalla Ayoub ni Muasisi wa ASP Jimbo la Mgogoni, Karibuni sana. (*Makofi*)

2. Pia tunae Mgeni wa Mhe. Omar Seif Abeid wa Jimbo la Konde, mgeni huyu ni Ndg. Marymam Rashid Juma, ambae ni Katibu wa CCM, Jimbo la Konde (*Makofi*) karibuni sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19. Hotuba hii inaambatana na uwasilishaji wa vitabu viwili; Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2017 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018; na kitabu cha Pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2018 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19. Taarifa za vitabu hivyo zimezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar wa Awamu ya Tatu (MKUZA III) 2016 na utatekelezwa hadi 2020. Mkakati huo umeandaliwa kwa kuzingatia pamoja na mambo mengine, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya mwaka 2015-2030 pamoja na Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein aliyoitoa kwenye uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba wa vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Ni wajibu wetu kama wanadamu kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, uzima, afya na uwezo wa kuweza kukutana ili kujadili mambo muhimu katika ujenzi wa Taifa letu kwa manufaa ya wananchi wote baada ya kumaliza mfunguo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hekima na busara katika mijadala ya kikao hiki na vyengine, atujaalie kheri, baraka na maelewano kati yetu. Atupe nguvu, utulivu, upendo na mshikamano miongoni mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee, naomba pia kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuongoza nchi ikiwa katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Jitihada na uoni wake mkubwa wa kuimarisha uchumi na kuinua huduma za jamii zinaonekana wazi katika

maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba. Huduma za maji, umeme, ujenzi wa barabara, elimu na afya ni miongoni mwa ahadi zake alizozitekeleza kwa ufanisi mkubwa sana. Hatuna budi ndugu wananchi, kuzilinda na kuzitunza rasilimali za nchi kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo *(makofi)*.
Mhe. Mwenyekiti, katika kuliendeleza Taifa na kusimamia shughuli za Serikali, Mheshimiwa Rais anashirikiana na Msaidizi wake Mkuu, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa kumshauri vyema na kufanya kazi kwa karibu sana na Mheshimiwa Rais. Kupitia fursa hii naomba pia kuwashukuru wajumbe wote wa Tume ya Mipango kwa kazi kubwa wanayofanya na ya Kikatiba. Miongozo na maelekezo yao yametusaidia sana katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango Mikuu ya Maendeleo ya Kitaifa ikiwemo ya kiuchumi, uwekezaji na kijamii ili kuimarisha na kuinua maslahi ya nchi yetu na kupunguza tatizo la umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nimshukuru Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid kwa kusimamia na kuendesha vyema vikao vya Baraza letu kwa ufanisi mkubwa. Hii inaonesha wazi ujasiri na umahiri alionao katika kuendesha shughuli za Baraza. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima, busara na ueledi katika utendaji wa kazi zake za kila siku. Napongeza pia ushirikiano madhubuti, hekima na busara tunazozishuhudia kutoka kwa wasaidizi wake akiwemo Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na wewe Mhe. Mwenyekiti Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi (*Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa imani yake kubwa kwangu na kuendelea kunikabidhi dhima ya kuwa msaidizi wake kwa masuala ya Fedha na Mipango. Najua kuwa dhima hii inanihitaji kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa kufuata sera na miongozo na sheria ziliopo na nitekeleze majukumu yangu kwa mujibu wa sheria na kwa maslahi ya Taifa. Namuomba Mola Muweza aniwezeshe kuyatekeleza yote hayo kwa uadilifu na ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nasimama katika Baraza hili kutokana na imani ya wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Donge. Niruhusu pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Donge kwa ushirikiano yao na mawazo wanayonipa na ustahamilivu wao mkubwa kwangu. Vile vile naishukuru sana familia yangu kwa kuwa na mimi muda wote, kunipa moyo, kuniunga mkono na kunisaidia kufanikisha majukumu niliyopewa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi na shukrani naomba nianze kwa kuwasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2017 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2017 hadi Machi mwaka 2018, lakini viile vile niwasilishe mwelekeo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2017

Mwenendo wa Uchumi

Hali ya Uchumi Duniani

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Uchumi Duniani, uchumi wa dunia umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2017, ikiwa ni kasi kubwa ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2016. Ukuaji kwa makundi tofauti ya nchi ni kama ifuatavyo: -

i. Nchi zilizoendelea kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 2.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2016. Ukuaji huo umechangiwa na kuimarika kwa biashara za kimataifa na kuongezeka kwa uzalishaji na usafirishaji wa nishati ya mafuta kwa nchi wazalishaji.

ii. Katika nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi kasi ya ukuaji wa uchumi ilifikia wastani wa asilimia 4.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2016. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji viwandani hasa kwa bidhaa zinazotumia malighafi ya chuma.

iii. Kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara uchumi umeendelea kukuwa kwa kasi ndogo pamoja na kujitokeza kuimarika kwa ukuaji wa wastani wa asilimia 2.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2016, hii inatokana na kuongezeka kwa bei ya nishati ya mafuta kwa nchi wazalishaji na kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ya kilimo katika hali ya kawaida, uchumi wa nchi hizo ambazo zipo nyuma, ulipaswa kukuwa kwa kasi kubwa zaidi ya nchi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi.

iv. Nchi za Afrika ya Mashariki, kasi ya ukuaji imeongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2017 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2016. Hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao na kuimarika kwa uwekezaji katika sekta ya miundombinu ya barabara na mawasiliano.

Mwenendo wa Mfumko wa Bei wa Dunia

Mhe. Mwenyekiti**,** Kwa mwaka 2017, kasi ya mfumko wa bei duniani imepanda na kufikia asilimia 3.2 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2016. Hii imetokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa za mafuta, madini ya chuma na huduma. Hata hivyo, kupanda kwa mfumko wa bei duniani kumeonesha ishara tofauti kwa baadhi ya maeneo kama ifuatavyo: -

i. Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi zilizoendelea imepanda hadi kufikia asilimia 1.5 kutoka asilimia 0.8 mwaka 2016 kutokana na kuongezeka kwa bei za mafuta na madini ya chuma;

ii. Katika nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi, kasi ya mfumko wa bei imepungua kufikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2016. Hii imetokana na udhibiti wa kasi ya mfumko wa

bei kwa nchi ya China na India na kuimarika kwa sarafu za baadhi ya nchi ikiwemo nchi ya Brazil;

iii. Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya mfumko wa bei imepungua kufikia asilimia 11.0 mwaka 2017 kutoka asilimia 12.8 mwaka 2016. Kuimarika kwa thamani ya sarafu kwa baadhi ya nchi ikiwemo nchi ya Angola na Nigeria ambazo ni wazalishaji na wasafirishaji wa nishati ya mafuta kumepelekea kupunguza kasi ya mfumko wa bei katika eneo hilo;

Katika nchi za Afrika ya Mashariki kasi ya mfumko wa bei imepungua hadi asilimia 6.1 mwaka 2017 kutoka asilimia 7.3 mwaka 2016 hii ni kutokana na kuongezeka kwa mavuno kutokana na hali nzuri ya hewa na kupungua kwa maradhi ya mimea.

Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika. Kwa mwaka 2017, Pato halisi la Taifa lilifikia thamani ya TZS 1,363 bilioni kutoka TZS 1,268 bilioni mwaka 2016. Juhudi za kuimarisha uchumi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zinaleta mafanikio katika kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kiuchumi. Ongezeko hilo la Pato la Taifa kwa mwaka 2017, linamaanisha kuwa Uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na mwaka 2016. Kasi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 baina ya mwaka 2015 na mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Sekta ya Kilimo imeongoza kwa ukuaji na kufikia wastani wa asilimia 8.8 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2016. Sekta ya Huduma nayo imekua kwa wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2016 na Sekta ya Viwanda imekua kwa asilimia 7.9 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 9.7 mwaka 2016. Shughuli zilizoongoza na kukuwa kwa kasi kubwa zaidi ni pamoja na sekta ndogo za Mazao ambayo ilikuwa (asilimia 18.9), Malazi na chakula ilikuwa kwa (asilimia 32.4), Malazi peke yake ni (asilimia 36.8), Utawala na Usaidizi (asilimia 28.3), Uchimbaji mawe (asilimia 25.1), Sanaa, Uburudishaji na Ubunifu (asilimia 36.2) na Usarifu wa Bidhaa Viwandani (asilimia 12.6).

Mchango wa Sekta katika Pato laTaifa

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia thamani ya kila sekta katika Pato la Taifa, Sekta ya Huduma inaendelea kuwa na mchango mkubwa ambapo mwaka 2017 ilichangia asilimia 44.4, ikifuatiwa na Sekta ya Kilimo asilimia 27.9 na Sekta ya Viwanda iliyochangia asilimia 17. Sekta ndogo zilizoonesha kuwa na mchango mkubwa zaidi ni pamoja na: mazao (asilimia 17.8), Malazi na Chakula (asilimia 11.5) na Ujenzi (asilimia 7.7).

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mambo yaliosababisha ukuaji mzuri wa uchumi wa asilimia 7.5 ni pamoja na haya yafuatayo:

i. Kuongezeka kwa Idadi ya Watalii waliofika nchini kwa asilimia 15.2 kufikia watalii 433,474 mwaka 2017 kutoka watalii 376,242 mwaka 2016;

ii. Kuongezeka kwa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi kwa asilimia 51.5 na kupunguza nakisi ya biashara kutoka asilimia 38.1 mwaka 2016 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017;

iii. Kuongezeka kwa kiwango cha uwekezaji binafsi kufikia thamani ya Dola za Kimarekani 437.8 milioni mwaka 2017 ikilinganishwa na thamani ya Dola za Kimarekani 150.5 milioni mwaka 2016;

iv. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kufikia jumla ya tani 324,106 mwaka 2017 ikijumuisha ongezeko la uzalishaji wa zao la mpunga kutoka tani 3,344 mwaka 2016 na kufikia tani 39,682.7 mwaka 2017.

v. Kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la biashara la karafuu kutoka tani 4,679 zenye thamani ya TZS 65,575 milioni mwaka 2016 kufikia tani 8,277 zenye thamani ya TZS 115,530 milioni mwaka 2017 na kuongezeka kwa ununuzi wa zao hilo kwa wakulima kutoka TZS. 65.5 bilioni mwaka 2016 kufikia thamani ya TZS. 115.5 bilioni mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 76.3.

vi. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini.

Pato la Mwananchi

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia makisio ya idadi ya watu wa Zanzibar 1,534,291 mwaka 2017 kutokana na Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 matokeo hayo ya uchumi wetu kwa mwaka 2017 yanamaanisha kuwa wastani wa Pato la Mtu binafsi limefikia TZS 2,021,000 sawa na Dola za Kimarekani 907 ikilinganishwa na TZS 1,806,000 sawa na Dola za Kimarekani 830 mwaka 2016.

Mwenendo wa Mfumko wa Bei wa Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa ikitumia jitihada mbali mbali za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kutokana na athari zake kwa wananchi na uwekezaji. Kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini imeshuka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2017 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2016. Kushuka huko kumesababishwa na kushuka kwa mfumko wa bei za bidhaa za chakula kufikia asilimia 5.5 kutoka asilimia 8.4 mwaka 2016. Hata hivyo, kasi ya mfumko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula, imepanda na kufikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2017 kutoka asilimia 4.8 mwaka 2016 kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa za mafuta katika soko la dunia.

Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania

Mhe. Mwenyekiti, Shilingi ya Tanzania imeshuka thamani kidogo kwa asilimia 2.4 katika kipindi cha mwaka 2017 ikilinganishwa na mwaka 2016, ambapo imebadilishwa na Dola ya Kimarekani kwa wastani wa TZS 2,229 mwaka 2017 kutoka wastani wa TZS

2,177 mwaka 2016 sawa na tofauti ya wastani wa TZS 52 ikilinganishwa na tofauti ya miaka miwili iliyopita (2016-2015) kwa tofauti ya wastani wa TZS 180.

Sekta ya Nje

Biashara na Nchi za Nje

Mhe. Mwenyekiti, kuongezeka kwa usafirishaji kwa mwaka 2017 kumesababisha kupungua kwa nakisi ya Biashara kwa asilimia 7.3 kutoka asilimia 38.1 mwaka 2016. Thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka kwa asilimia 51.5 kutoka thamani ya TZS 96.2 bilioni mwaka 2016 kufikia thamani ya TZS 145.7 bilioni mwaka 2017. Ongezeko hilo limetokana na usafirishaji wa zao la karafuu kutoka tani 3,721 zenye thamani ya TZS 64.7 bilioni kwa mwaka 2016 na kufikia tani 7,077 zenye thamani ya TZS 121.8 bilioni mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umeongezeka kwa asilimia 26.6 kutoka TZS 167.0 bilioni mwaka 2016 kufikia TZS 211.4 bilioni mwaka 2017. Uagiziaji huo wa bidhaa unahusisha bidhaa kama vile mashine, vifaa vya umeme, vyombo vya moto na vipuri.

Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya thamani ya uhaulishaji wa bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara imefikia thamani ya TZS 240.1 bilioni. Kati ya uhaulishaji huo bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar zimeongezeka kufikia thamani ya TZS 206.5 bilioni mwaka 2017 kutoka thamani ya TZS 138.0 bilioni mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 49.6. Aidha, Uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umepungua kutoka thamani ya TZS 84.7 bilioni mwaka 2016 kufikia thamani ya TZS 33.6 bilioni mwaka 2017 sawa na upungufu wa asilimia 60.4.

Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya utalii imeendelea kuongoza katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Sekta hii inaendelea kusaidia upatikanaji wa ajira na kukuza biashara kwa bidhaa za asili na uingizaji mapato ya fedha za kigeni na mapato ya Serikali. Kuimarika kwa masoko yaliopo na mapya ya watalii kumepelekea kuongezeka kwa uingiaji wa watalii nchini kwa asilimia 15.2 kutoka watalii 376,242 mwaka 2016 na kufikia watalii 433,474 mwaka 2017.Watalii wengi waliotembelea Zanzibar ni kutoka nchi za Italia, Ujerumani, Uingereza na Israel.

Uwekezaji Binafsi Kupitia ZIPA

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia mamlaka ya kukuza vitega uchumi (ZIPA) inaendelea na jitihada za kushajihisha uekezaji wa kutoka nje na ndani ili kujenga wigo madhubuti wa kiuchumi. Kiwango cha uwekezaji binafsi kilipanda hadi thamani ya Dola za kimarekani 437.7 milioni mwaka 2017 kutoka thamani ya Dola za Kimarekani 150.5

Milioni mwaka 2016 hii ni sawa na ongezeko la asilimia 191. Kuongezeka kwa uwekezaji binafsi nchini kumetokana na uwekezaji mkubwa katika sekta za Hoteli za kitalii na mikahawa, Kilimo, Uwindaji na Misitu, Ukodishaji Majengo na biashara na Uvuvi. Kuongezeka kwa Miradi binafsi ya uwekezaji kumepelekea kuongezeka kwa idadi ya ajira kutoka 1,071 mwaka 2016 kufikia ajira 1,557 mwaka 2017.

Mapato na Matumizi ya Serikali

Mapato ya Ndani

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya mapato ya ndani yanayokusanywa yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2013/2014 yalikuwa ni TZS 350.6 bilioni na kufikia TZS 675.8 bilioni mwaka 2017/2018. Sawa na ongezeko la asilimia 92.8 kwa kipindi hicho. Hii imetokana na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji kodi iliopelekea kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali ilikadiria kukusanya mapato kutokana na vyanzo vya ndani jumla ya TZS 675.8 bilioni sawa na asilimia 21.8 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 627.0 bilioni zitatokana na makusanyo ya vyanzo vya kodi na TZS 48.8 bilioni ni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2017 hadi Machi 2018) mapato ya ndani yalifikia TZS 506.6 bilioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka ya TZS 675.8 bilioni. Ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 jumla ya TZS 389.6 bilioni zilikusanywa katika kipindi kama hicho na kuonesha ukuaji wa mapato ya TZS 117 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 30. Kati ya makusanyo hayo, mapato kutokana na kodi yalifikia TZS 465.2 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 74.2 ya makadirio ya mwaka ya TZS 627 bilioni. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 41.4 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka ya TZS 48.8 bilioni.

Matumizi ya Serikali 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2017 hadi Machi 2018) mwaka wa Fedha 2017/18 jumla ya TZS 1,087 bilioni zimekadiriwa kutumika. Kati ya matumizi hayo yaliyokadiriwa, TZS 590.7 bilioni ni kwa Kazi za Kawaida na TZS 496.6 bilioni ni kwa Kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018 matumizi halisi yalifikia TZS 676.9 bilioni sawa na asilimia 62 ya makadirio ya mwaka. Kati ya matumizi hayo TZS 457.1 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida na TZS 219.8 bilioni zilitumika kwa kazi za maendeleo.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018 ni muendelezo wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Awamu ya Tatu (MKUZA III) unaotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano hadi 2021.

Kwa mwaka 2017/2018, Mpango wa Maendeleo umelenga kutekeleza jumla ya programu 27 (programu mbili mpya) na miradi 46 (miradi 11 mipya) ya maendeleo.

Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya TZS 496.6 bilioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo Serikali ilipanga kutumia jumla ya TZS 116.1 bilioni, sawa na asilimia 23.7 ya bajeti ya maendeleo kutokana na fedha za ndani na TZS 380.5 bilioni sawa na asilimia 76.3 zimepangwa kutokana na ruzuku na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa utekelezaji halisi, hadi mwisho wa mwezi wa Machi 2018, jumla ya TZS 219 bilioni zilitumika sawa na asilimia 44 ya bajeti ya maendeleo ambapo TZS 70.4 bilioni zilitolewa na Serikali sawa na asilimia 61 na TZS 151 bilioni sawa na asilimia 40 zilitolewa na Washirika wa Maendeleo.

UTEKELEZAJI WA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2017/18

Mhe. Mwenyekiti, serikali iliendelea kuvitekeleza vipaumbele vya mwaka wa 2017/18 ili kufikia malengo ya maendeleo ya nchi. Utekelezaji wa maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Kuimarisha Miundombinu ya Maeneo ya Uingiaji Nchini (Yanayojumuisha Bandari na Viwanja vya Ndege), Barabara pamoja na Nishati:

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha miundombinu ya uingiaji nchini, barabara na nishati, miradi kadhaa ya kuendeleza miundombinu ya msingi ilipangwa na kutekelezwa. Maendeleo ya utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

i. Ujenzi wa Jengo jipya la abiria *(Terminal III):* Mradi huu ulikwama utekelezaji wake kwa muda mrefu kutokana na mahitaji ya ziada ya fedha, hatimae ufumbuzi wa changamoto hiyo umepatikana kwa Benki ya Exim ya China kukubali kufadhili mahitaji hayo ya ziada kupitia mkopo nafuu. Shughuli za ujenzi wa maegesho ya ndege kwa maana ya (*apron*), magari (*parking*) pamoja na jengo zinaendelea baada ya mkandarasi na mshauri elekezi kurudi kwenye eneo la mradi na kuendelea na kazi.

ii. Ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado zinaendelea na hatua za utekelezaji wa mradi huo. Hata hivyo, Serikali zimekubaliana kufanya mapitio ya upeo wa mradi kwa maana ya *(Scope)* na gharama zake ili kujiridhisha na kiwango hicho au kutumia njia mbadala ya kugharamia.

iii. Ununuzi wa meli mbili ya mafuta na abiria/mizigo: matayarisho ya ujenzi wa meli mpya ya mafuta yameanza ambapo mkataba umesainiwa na malipo ya mwanzo ya asilimia 30 yamefanyika.

iv. Ujenzi wa barabara za Bububu - Mahonda – Mkokotoni: malipo ya fidia kwa nyumba na vipando vilivyopo katika eneo litakaloathirika na ujenzi kutoka Chuini kwa Nyanya hadi Mkokotoni umefanyika. Aidha, Mkandarasi ameanza kuleta vifaa vya ujenzi wa barabara na kujenga makaazi na ofisi katika eneo la Kandwi.

v. Ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja (35 km): Ujenzi unaendelea ambapo kilomita 7 kutoka Ole mpaka Vitongoji zimeshawekwa lami na ujenzi wa makalavati manne eneo la Changaweni Fidel Castro umefanyika. Tabaka la mwisho kabla ya kuweka lami kwa kilomita 4.7 kutoka Mfikiwa hadi Pujini na usafishaji kutoka Kichaka mpaka Kendwa vimekamilika.

vi. Upelekaji wa umeme katika Kisiwa cha Uvinje: Mradi huo wa kuutoa umeme kutoka Kisiwa cha Fundo umeanza na usafishaji wa eneo litakalopita umeme lenye urefu wa kilomita 2.2 katika visiwa hivyo umekamilika.Tathmini inaendelea kwa watakaoathirika katika mradi huo ili kuweza kulipwa fidia zao. Visiwa hivyo vitaunganishwa kwa kutumia nguzo (*overhead line*) zenye urefu wa kilomita 4.5 badala ya kupitia chini ya bahari.

vii. Utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia: Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Serikali iliendelea na hatua kadhaa za utafiti wa mafuta na Gesi Asilia kwa kufanya shughuli mbali mbali kwa kuanzia na uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa awali kwa njia ya anga *(Full Tensor Gravity Survey - FTG),* iliyofanyika kuanzia tarehe 14.03.2017 kwa maeneo ya Kitalu cha Pemba kwa madhumuni ya kuangalia miamba yenye uwezo wa kuhifadhi Mafuta na gesi asilia. Uchambuzi huo unafanywa na Kampuni ya *BELL GEOSPACE* ya Scotland chini ya mkataba na Kampuni ya *RAK GAS International* ya Umoja wa Falme za Kiarabu na umesaidia kupatikana maeneo ya utafiti kwa njia ya mtetemo kwa upande wa baharini na nchi kavu unaofanywa na Kampuni ya *BGP* kutoka nchini China. Kampuni hiyo ya *BGP* ilianza utafiti tarehe 28.10.2017.

Mkakati wa Utafutaji Rasilimali Fedha:

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeanza mchakato wa ununuzi wa mashine za elektroniki za kutolea risiti. Zabuni ya kwanza ilifutwa kwa sababu ya kukosekana ushindani na kupelekea zabuni kutangazwa upya ambayo kwa sasa ipo katika hatua ya tathmini.

Kuimarisha Viwanda Vidogo Vidogo kwa Kuongeza Thamani Bidhaa na Ubora wa Vifungashio:

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio yafuatayo yalitekelezwa:

i. Vifaa vya uvunaji na usarifu wa mwani vyenye thamani ya TZS 175 milioni sawa na Dola za Marekani 78,000 vimetolewa kwa wakulima wa mwani ikiwa ni msaada kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Viwanda *(UNIDO).*

ii. Ujenzi wa jengo moja (kati ya mawili) la Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa ajili ya kupima ubora wa bidhaa na huduma unaendelea na umefikia katika ghorofa ya pili.

Kuimarisha Kilimo kwa Kujenga Miundombinu ya Umwagiliaji Maji, Uvuvi na Mifugo

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo yafuatayo yamefanyika:-

i. Shughuli za uhifadhi wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji maji umefanyika kupitia ujenzi wa matuta katika skimu tatu ambazo ni Uzini, Muyuni kwa Unguja na Kisaani kwa Pemba;

ii. Jumla ya mita 480 ya misingi ya umwagiliaji maji imejengwa kwa kiwango cha saruji katika mabonde ya Bumbwisudi (mita100), Uzini (mita 180) na Kibokwa (mita 200);

iii. Uchimbaji wa visima viwili katika bonde la Cheju umekamilika;

iv. Ujenzi wa kituo cha kulelea na kutotolea vifaranga vya samaki Bait el Ras unaendelea ambapo jengo jipya la kufugia vifaranga limekamilika, mabwawa matatu ya kufugia samaki nayo pia yamekamilika. Aidha, matengenezo ya majengo ya zamani yanaendelea. Zabuni kwa ununuzi wa gari mbili za mradi imeshatangazwa;

v. Uendelezaji uvuvi wa bahari kuu umeanza kwa kuanzishwa Kampuni ya Uvuvi (*ZAFICO*) inayomilikiwa na mashirika ya serikali. Mchakato umeanza wa ununuzi wa boti mbili za uvuvi pia hatua za awali za kutengeneza vyumba vya barafu katika eneo la *ZAFICO* lililopo Malindi zimeanza. Kwa upande mwengine Serikali ya Mapinduzi imekubaliana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ili kuyawezesha makampuni kutoka China kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu pamoja na ujenzi wa viwanda vya kusarifu samaki. Kwa kuanzia kampuni tatu; *CRCC, Hong Dong* na *Putian Fisheries* zimeonesha nia ya kuekeza katika Sekta hii ya Uvuvi.

vi. Taasisi ya utafiti wa mifugo imeendelea kuimarishwa kwa kuipatia vifaa na wataalamu.

Kuimarisha Ubora wa Huduma za Kijamii Zikiwemo Elimu, Afya, Michezo na Upatikanaji wa Maji Safi na Salama:

Mhe. Mwenyekiti, ili kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama yafuatayo yameweza kufanyika.

i. Ujenzi wa skuli tisa za ghorofa kwa ngazi ya Sekondari Unguja na Pemba unaendelea kwa hatua mbali mbali. Skuli hizo ni: Mwembeshauri, Bububu, Kinuni, Fuoni na Chumbuni kwa Unguja na Wara, Micheweni, Kizimbani na Muwambe kwa Pemba;

ii. Hospitali ya Kivunge inaendelea kuimarishwa na kupandishwa hadhi kuwa ya Wilaya, kwa kufanya matengenezo ya wodi ya watoto na wodi ya wazazi katika hospitali hiyo. Aidha, kwa upande wa kuimarisha mfumo wa uhifadhi wa damu salama kwa mama na mtoto vifaa muhimu ikiwemo chumba cha baridi (*cold room*) vimeagizwa;

iii. Ujenzi wa vituo vipya vya afya viwili na matengenezo makubwa kwa vituo vya afya 13 unaendelea kwa hatua mbali mbali. Vituo vinane kwa upande wa Unguja vimekamilika ikiwemo uwekaji wa vifaa vinavyohitajika. Kwa upande wa Pemba, jumla ya vituo sita viko katika hatua za umaliziaji.

iv. Matayarisho ya ujenzi wa wodi ya wazazi (*maternity block*) na wodi ya watoto (*paediatric block*) katika hospitali ya Chake Chake yameanza kwa kutayarisha michoro na mkataba wa kazi hiyo kati ya mkandarasi na wizara umeshawekwa saini;

v. Kwa upande wa ujenzi wa nyumba za madaktari katika hospitali ya Abdalla Mzee, upembuzi yakinifu umekamilika na kazi ya kuandaa michoro inaendelea;

vi. Upimaji na uwekaji wa nguzo katika eneo la hospitali ya Binguni umekamilika. Majengo yaliyojengwa katika eneo hilo na *African Muslim Agency* tayari yamekabidhiwa Wizara ya Afya. Hatua inayofuata ni kufanya tathmini ya gharama za matengenezo ya majengo ili kuiwezesha Taasisi ya Utafiti - *Zanzibar Institute of Health Research* (*ZIHR*) kuhamia katika majengo hayo;

vii. Jengo la Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali limekamilika. Taratibu za ununuzi wa samani za maabara pamoja na mashine za kufanyia uchunguzi zinaendelea;

viii. Visima 26 kati ya 150 vilivyochimbwa kwa msaada wa Ras Al Khaimah vilivyoko katika maeneo mbali mbali vipo katika hatua mbali mbali za uendelezaji ikiwemo uwekaji wa *well-head*, uvutaji wa umeme, ujenzi wa vibanda vya pampu na utandazaji wa mabomba. Jumla ya visima 6 vimekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi. Visima hivyo ni Mbweni (*ZSSF*), Mitakawani, Mtambwe-Mivumoni, Ngwachani, Kiwani, na Kifundi.

ix. Matayarisho ya ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya vimeanza kwa kufanya utafiti wa kimazingira na kufanya utafiti wa udongo kwa Micheweni eneo la Kishindeni na Mkoani eneo la Kangani Pemba. Aidha, ujenzi wa kiwanja cha michezo cha Mao Tze Dong unaendelea kwa shughuli mbalimbali ikiwemo; uwekaji wa majani bandia katika kiwanja cha mpira wa miguu pamoja na viwanja vya michezo ya ndani na michezo mchanganyiko.

Utawala Bora na Uimarishaji wa Taasisi, Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Uwekaji Mji Katika Hali ya Usalama:

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha utawala bora na uimarishaji wa taasisi, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uwekaji mji katika hali ya usalama, yafuatayo yameweza kufanyika:

i. Rasimu ya awali ya miongozo ya uimarishaji wa taasisi kwa ajili ya kupeleka madaraka kwa wananchi imetayarishwa na kuwasilishwa serikalini ambapo mapendekezo yameanza kufanyiwa kazi. Miongozo hiyo ni (i) Kujenga Uwelewa wa Masuala ya Ugatuzi na Mawasiliano; (ii) Kujenga uelewa kwa maeneo ya Ugatuzi wa Kifedha; (iii) Kuoanisha Sera na Sheria; (iv) Rasilimali Watu; na (v) Miundo ya Kitaasisi.

ii. Ujenzi wa majengo ya Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa upande wa Pemba umekamilika. Shughuli zinazoendelea ni ukamilishaji kwa kuweka huduma za umeme, maji, TEHAMA, kamera za *CCTV* na simu za ndani pamoja na fremu za milango;

iii. Utayarishaji wa michoro ya jengo la nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba umekamilika pamoja na kutayarisha gharama za ujenzi (*BoQ*) na kukabidhiwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa ajili ya ujenzi;

iv. Kwa upande wa KMKM, ujenzi wa jengo la utawala na hanga moja katika kambi ya Kojani umekamilika. Hatua za ukamilishaji zinaendelea. Kwa upande wa Makombeni, hatua za ujenzi wa majengo umeanza na unatarajiwa kukamilika Julai 2018.

v. Katika kambi ya Chuo cha Mafunzo ya Tungamaa, majengo matano yamekamilika hadi kuezekwa. Aidha, ujenzi wa nyumba sita umekamilika hadi hatua ya kuezeka katika kambi ya Kengeja;

vi. Uwekaji kamera na vifaa vya ulinzi katika maeneo ya Mji Mkongwe na maeneo mengine ya mjini unaendelea. Nyingi ya kamera hizo zimeshaunganishwa na Kituo cha Kupokelea Mawasiliano (*Control and*

Command Centre) na kuanza kazi ambapo ukusanyaji wa taarifa na kumbukumbu za matukio ya kijamii unaendelea;

vii. Mradi wa Huduma za Jamii Mijini Zanzibar (*ZUSP*) unaendelea na ujenzi wa misingi ya maji ya mvua kama ifuatavyo: Eneo la Jang'ombe (*system E*) lenye urefu wa mita 1700 umefikia asilimia 95, na eneo la Kwamtipura (*system I*) lenye urefu wa mita 2400 limekamilika. Ujenzi kwa maeneo ambayo hayahitaji ulipaji wa fidia umeanza kwa ajili ya msingi wa maji ya mvua wa *system C. System* hii ina madhumuni ya kuondosha maji yaliyopo katika ziwa la Mwanakwerekwe na unaanzia Magogoni kupitia Sebleni, Kibanda Maiti, na Kwa Abbass Hussein na kuishia baharini. (*Makofi*)

MASUALA MTAMBUKA

Udhalilishaji:

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea na kumwezesha mwanamke kiuchumi, kisiasa na kijamii pamoja na kupinga ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Aidha, serikali imeendelea na kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto nchini kupitia mambo mbali mbali ambayo yamefanywa na serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imezindua mpango kazi wa miaka mitano wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto na Kamati 24 za kupinga Ukatili na Udhalilishaji (12 Unguja na 12 Pemba) zimejengewa uwezo juu ya dhana ya ukatili wa kijinsia.Timu 11 za viongozi wa dini 88 (55 Unguja na 33 Pemba) kwa Wilaya zote Unguja na Pemba zimewezeshwa kutekeleza shughuli za kuelimisha jamii kupitia vikao mbali mbali vya kidini. Jumla ya watu 31,152 (22,873 Unguja na 8,279 Pemba) wamepatiwa taaluma.

Upelekaji wa Madaraka kwa Wananchi Kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa:

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwaka wa fedha 2017/18, baadhi ya majukumu ya Sekta za Elimu, Afya na Kilimo yameanza kusimamiwa na kutekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hatua hii ni utekelezaji wa maamuzi ya serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa katika mipango mikuu ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maendeleo yaliyofikiwa, kuna changamoto mbali mbali zinazokabili utekelezaji wa masuala ya ugatuzi zikiwemo uhaba wa nafasi za ofisi kwa watumishi wanaohamishiwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ingawa juhudi zinafanyika za kupanua majengo ya ofisi ili kukidhi mahitaji. Kwa mwaka 2018/19, serikali itaendelea na hatua za ugatuzi wa wafanyakazi wanaotarajiwa kupelekwa katika Halmashauri na suala la kujenga uelewa juu ya masuala ya ugatuzi litaendelea kupewa umuhimu unaostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendelea kusimamia ukamilishaji wa miongozo itakayotumika katika utekelezaji wa shughuli za ugatuzi katika uandaaji wa mipango na bajeti; uhamisho wa watumishi kutoka sekta zilizogatuliwa; majukumu na mahusiano baina ya sekta, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na mipaka ya ukusanyaji wa mapato baina ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Miundo ya kitaasisi itakayokidhi matakwa ya ugatuzi itasimamiwa ukamilishaji wake pamoja na uandaaji wa Mkakati wa Mawasiliano.

Utafiti wa Nishati Inayorejesheka (Jua na Upepo):

Mhe. Mwenyekiti, matokeo ya ripoti ya utafiti wa awali wa mwezi Agosti, 2017 yameonyesha kuwa wastani wa kiwango cha nguvu za jua kwa siku ni **5.75** *KWH (Kilo Watt Hour).* Hii inathibitisha kuwepo kwa kiwango cha jua cha kutosha nchini kuendelea na uwekezaji katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu ya jua.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na matokeo hayo ya kuridhisha kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na kupima maeneo ya uwekezaji wa mitambo ya uzalishaji umeme kwa kutumia jua kwa maeneo ya Makunduchi, Bambi, Matemwe, Muwambe na Micheweni. Uwekezaji katika miundombinu ya uzalishaji kwa kutumia upepo utafanyika baada ya kukamilika kwa utafiti unaoendelea kwa kipindi cha mwaka mmoja. Ikumbukwe kwamba kukamilika kwa utafiti huu kutaiwezesha Zanzibar kuwa na vyanzo mbadala vya uzalishaji wa umeme kutoka katika vyanzo salama na rafiki kwa mazingira hali ambayo itakubaliana na uendelezaji wa sekta ya utalii na kulinda mazingira kwa ujumla. Kazi nyengine zinazoendelea ni kutoa elimu kwa wananchi na wataalamu wazalendo juu ya teknolojia hiyo kwa lengo la kuongeza uelewa na kuwajengea uwezo katika uwekezaji huo.

Masuala ya Idadi ya Watu:

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na udogo wa idadi ya watu katika nchi yetu, tumekabiliwa na changamoto ya kasi kubwa ya ongezeko ya idadi hiyo kutokana na sababu mbali mbali.

Kwanza ni matumizi madogo ya njia za uzazi wa mpango. Kwa mujibu wa utafiti wa kidemografia na afya wa 2015/16, kiwango cha utumiaji wa njia za kisasa za uzazi wa mpango kwa Zanzibar ni asilimia 14 ambacho ni kidogo sana. Hali hii inachangiwa na muamko mdogo kwa wanaotumia huduma hizi na kutoshiriki kwa wanaume katika masuala ya uzazi wa mpango. Matokeo yake, Zanzibar ina kiwango kikubwa cha uzazi kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa (miaka 15 – 49). Kwa mujibu wa utafiti huo mwanamke mmoja alie katika umri wa kuzaa kwa wastani huzaa watoto 5.1. Ili kurekebisha changamoto hii ipo haja kwa jamii kubadili mtazamo wake juu ya matumizi ya njia za uzazi wa mpango, kutolewa elimu hasa kupitia viongozi wa dini na kuhamasisha wanaume kushiriki katika kupatiwa elimu ya uzazi na umuhimu wa kutumia uzazi wa mpango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine, serikali kupitia Tume ya Mipango inaendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya Idadi ya Watu ya Zanzibar ya mwaka 2008. Kazi hiyo ipo katika hatua za mwisho kukamilika na imeshirikisha wadau mbali mbali kutoka serikalini na sekta binafsi ambayo maoni yao yamesaidia kuifanya rasimu ya sera hiyo kuwa bora zaidi. Hatua inayofuata ni kukamilisha rasimu ya mwisho ya sera hiyo na kuiwasilisha rasmi serikalini kwa kuidhinishwa.

Miradi ya Mashirikiano Baina ya Sekta za Umma na Binafsi:

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeridhia kufanyika kwa Upembuzi yakinifu kwa miradi 13 ambayo iko katika hatua mbali mbali za maandalizi. Miradi hiyo ni:- (i) Miradi mitano ya ujenzi na uendeshaji wa masoko. Masoko hayo ni Mwanakwerekwe, Mkokotoni, Mombasa, Kengeja na ChakeChake; (ii) Ujenzi wa kituo cha daladala Kijangwani; (iii) Ujenzi wa nyumba za bei nafuu eneo la Ng'ambo; (iv) Kuendeleza vivutio vya utalii eneo la Bandari ya Malindi; (v) Uendelezaji wa viwanda vya usarifu wa mazao ya kilimo na uvuvi; (vi) Ujenzi wa viwanja vya michezo; (vii) Ujenzi wa dakhalia za Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*); (viii) Mradi wa Bandari ya Mafuta na Gesi Mangapwani; na (ix) Mradi wa nishati mbadala ya jua. Mradi wa Bandari ya Mafuta na Gesi Mangapwani na mradi wa Nishati Mbadala ya jua upembuzi yakinifu wa awali umekamilika. Hatua inayofuata ni kufanya upembuzi yakinifu kamili ambao serikali imeshautolea maelekezo na mshauri wa kufanya kazi hiyo tayari ameshapatikana.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2018

Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

Mhe. Mwenyekiti, uchumi duniani unatarajiwa kukua kwa kasi kubwa zaidi ya wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2018 kutoka wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2017. Kwa mgawanyiko wa maeneo, mwenendo huo unatarajiwa kuwa kama ifuatavyo: -

i. Nchi zinazoendelea uchumi wake unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2018 kutoka wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2017. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea kutatokana na kuimarika kwa vitega uchumi, biashara, na uzalishaji viwandani hasa katika nchi za Ulaya;

ii. Nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2018 kutoka wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2017. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji na uzalishaji viwandani hasa katika nchi zinazoibukia kiuchumi kama vile China, Uturuki na Urusi;

iii. Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara uchumi wa nchi hizo unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.3 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji kwa wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2017. Inakadiriwa kuwa kupanda kwa bei kwa bidhaa za mafuta kutachangia

kukuza uchumi wa nchi hizo hasa nchi wazalishaji wa mafuta katika kanda hii wakiwemo Angola, Nigeria na Sudani ya Kusini. Vile vile, uchumi wa Afrika ya Kusini ambayo ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Afrika unatarajiwa kupanda kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji hasa katika maeneo ya nishati na madini.

Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar 2018:

Pato la Taifa:

Mhe. Mwenyekiti, Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2018 utaongozwa na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, MKUZA III pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Pato la Taifa kwa mwaka 2018 linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.7. Matarajio ya ukuaji wa uchumi yatatokana na mambo yafuatayo:

i. Kuongeka uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kuongezeka kwa matumizi ya pembejeo na matrekta 20 mapya;

ii. Kuimarika uwekezaji wa ndani na nje kwa kutekelezwa miradi mipya ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, uwanja wa ndege na makaazi, kwa upande wa makaazi hasa katika eneo la Kwahani na Chumbuni itakayotekelezwa kwa ubia kati ya *ZSSF* na Kampuni ya China *Nantong Sanjian Construction Group* (*CTNC*) kutoka China pamoja na miradi binafsi ya uwekezaji katika maeneo ya Nyamanzi ambayo inaendelea, Fumba, Mtoni, Matemwe, Micheweni na mengineyo;

iii. Kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji maji kwa ushirikiano na Serikali ya Korea;

iv. Kuongezeka kwa kiwango cha idadi ya watalii wanaoingia nchini kutokana na kuimarika kwa masoko yaliopo na masoko mapya ya utalii;

v. Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Viwanda;

vi. Kuanza utekelezaji wa mradi wa ufukiaji ardhi (*reclamation*) katika eneo la Kinazini (Pwani mbovu) hadi Mpigaduri kwa ajili ya mji mpya wa makaazi na biashara; na

vii. Kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu nchini.

Shabaha na Malengo ya Uchumi kwa Mwaka 2018:

Mhe. Mwenyekiti, shabaha na malengo ya uchumi kwa mwaka 2018 ni kama ifuatavyo: -

i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.7 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2017;

ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei katika tarakimu moja;

iii. Mapato ya kodi kuwa asilimia 21.8 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka asilimia 20.2 kwa mwaka 2017/18;

iv. Kupunguza nakisi ya bajeti kutoka asilimia 4.4 mwaka 2017/18 hadi asilimia 3 mwaka 2018/19; na

v. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu.

MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2018/19

Mhe. Mwenyekiti, serikali inaendelea kutekeleza Dira ya Maendeleo ya 2020 ikiwa ni kipindi chake cha mwisho cha miaka mitano kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA III). Katika kufanikisha hilo, serikali imeainisha miradi ya kimkakati (*Flagship projects*) kwa ajili ya utekelezaji wa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020. Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19 umezingatia utekelezaji wa miradi hiyo ya kimkakati pamoja na mengineyo iliyoibuliwa ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo na shabaha za Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020. Jumla ya programu tisa na miradi 10 ya kimkakati imepangwa kutekelezwa na imezingatiwa katika maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2018/19.

Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2018/19:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2018/19 maeneo yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni kama yafuatayo:

Kuimarisha Miundombinu ya Maeneo ya Uingiaji Nchini, Barabara na Nishati:

Mhe. Mwenyekiti, serikali inadhamiria kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar (*Terminal III*). Kuimarisha uwanja wa ndege wa Pemba ambapo upembuzi yakinifu umekamilika. Kwa mwaka 2018/19 serikali inakusudia kukipanua kwa kuongeza urefu na upana wa njia ya kutua na kurukia ndege (*run way*), kujenga njia mpya ya ndege kujitayarisha kuruka (*taxi way*), eneo la maegesho ya ndege (*apron*), jengo jipya la abiria (*Terminal II*) na ukuta ili kuimarisha usalama katika kiwanja hicho cha Pemba. Kiwanja kinatarajiwa kuwa na uwezo wa kupokea ndege za ukubwa wa *Boeing* 737-8. Jitihada za kutafuta fedha zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la bandari ya Mangapwani litaimarishwa kwa ujenzi na uwekaji wa miundombinu muhimu na ya msingi ikiwemo barabara, maji na umeme ili kutumika kwa ushushaji, upakiaji na uhifadhi wa Mafuta na Gesi. Sambamba na hayo, serikali itaendelea na ujenzi wa meli mpya na ya kisasa ya mafuta ili kuweza kukidhi mahitaji ya usafirishaji wa bidhaa hiyo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa upande wa usafiri wa barabara, serikali itaendeleza ujenzi wa barabara za Bububu-Mahonda na Mkokotoni zenye jumla ya (31km), Mkwajuni – Kijini (9.4km) na Matemwe – Muyuni (7.6km). Vile vile serikali itaendeleza barabara ya Fuoni - Kombeni (8.6km); Chake

Chake – Wete (22.1km); Pale – Kiongele (4.6km); Ole – Kengeja (35km). Aidha, upembuzi yakinifu kwa barabara za Chake Chake – Mkoani (31km), Tunguu - Makunduchi (30km) na Fumba – Kisauni (12km) utakamilika. Katika kuondosha tatizo la kujaa maji katika barabara mbali mbali, serikali itatengeneza madaraja katika maeneo ya Kibonde Mzungu na Mwanakwerekwe na ujenzi wa mitaro katika eneo la barabara ya Kiembe Samaki.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inaendelea na azma yake ya kujenga Bandari ya Mpigaduri ili iweze kuimarisha huduma za usafirishaji wa mizigo. Kwa mwaka 2018/19 itakamilisha mapitio ya upeo na gharama za mradi na kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuamua njia muafaka ya kugharamia utekelezaji wa mradi huo. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuanza mara tu mambo hayo pamoja na upatikanaji wa fedha utakapokamilika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya nishati, azma ya usambazaji wa umeme katika visiwa vidogo vidogo kutoka gridi ya taifa itaendelezwa. Serikali imekamilisha kupeleka nishati hiyo katika kisiwa cha Fundo na inakamilisha kupeleka umeme katika kisiwa cha Uvinje kwa mwaka 2017/18. Kwa mwaka 2018/19 inakusudia kuunganisha na kusambaza umeme katika kisiwa cha Kokota.

Kuendeleza Utalii

Mhe. Mwenyekiti, serikali inakusudia kuendeleza utekelezaji wa Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*R4P*) katika sekta ya utalii kwa kuimarisha maeneo ya kihistoria kwa kufanya matengenezo katika maeneo ya Fukuchani kwa Unguja na Mkamandume – Pemba. Aidha, inakusudia kuliendeleza eneo la Kwa Bihole kwa kuweka miundombinu, huduma za msingi na vivutio vyengine ili iwe kivutio kwa wenyeji na wageni wanaotembelea Zanzibar. Sambamba na hilo, serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Oman italifanyia matengenezo makubwa jengo la Beit-el-Ajaib ambalo ni kivutio kikubwa kwa watalii na ni alama muhimu kwa nchi yetu.

Kuimarisha Viwanda Vidogo Vidogo kwa Kuongeza Thamani Bidhaa na Ubora wa Vifungashio:

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarishsa viwanda vidogo vidogo Serikali imekusudia kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio. Mkazo umewekwa katika kuendeleza viwanda vidogo vidogo na vya kati kwa kuendelea kuhamasisha usarifu na kuongeza thamani za bidhaa sambamba na ununuzi wa mashine za usarifu wa mwani. Pia kufanya ukarabati wa majengo yalioko Maruhubi ili yaweze kuwa Makao Makuu ya Wakala wa Uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA) na kuanza taratibu za ujenzi wa ofisi na vituo vya Mikoa. Aidha, serikali imekusudia kuanzisha maeneo tengefu katika Wilaya zote Unguja na Pemba kwa kuyapima, kulipa fidia na kutayarisha Mpango Mkuu wa Viwanda. Sambamba na hayo, serikali imekusudia kukamilisha ujenzi wa maabara za Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*) na kazi inaendelea vizuri.

Kuimarisha Kilimo kwa Kujenga Miundombinu ya

Umwagiliaji Maji, Uvuvi na Mifugo:

Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendelea na juhudi za Uimarishaji wa kilimo cha umwagiliaji maji kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji hekta 720 katika mabonde ya Cheju, Kilombero, Kibokwa, Kinyasini, Chaani, Makwararani na Mlemele sambamba na ununuzi wa matrekta 10 pamoja na vifaa vyake. Aidha, serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inakusudia kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi *(Fish landing Port)* sambamba na ujenzi wa kituo cha kupokelea na kulelea vifaranga vya samaki eneo la Chokocho Pemba, ununuzi wa vifaa pamoja na utoaji wa taaluma kwa wafugaji. Kampuni ya Uvuvi (*ZAFICO*) itakamilisha ununuzi wa boti mbili za uvuvi wa bahari kuu. Kwa mashirikiano na kampuni mbali mbali za nje zikiwemo *CRCC*, *Hong Dong* na *Putian Fisheries* kutoka China ambazo tayari zimeonesha mashirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu lakini vile vile kujenga viwanda vya usarifu wa mazao ya baharini.

Kuimarisha Ubora wa Huduma za Kijamii zikiwemo Elimu, Afya, Makaazi, Michezo na Upatikanaji wa Maji safi na Salama:

Mhe. Mwenyekiti, katika sekta ya elimu mkazo umewekwa katika kuimarisha miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukamilisha ujenzi wa madarasa 140 yaliyoanzishwa na wananchi, sambamba na kukamilisha ujenzi wa skuli tisa za Ghorofa za sekondari (Mwembeshauri, Kinuni, Fuoni, Bububu na Chumbuni kwa Unguja, Micheweni, Wara, Mwambe na Kizimbani kwa Pemba); pamoja na kuanza ujenzi wa maabara kwa skuli 23 za sekondari na madarasa 48 mapya katika skuli sita za Sekondari (Unguja 4 na Pemba 2) pamoja na ununuzi wa samani. Aidha, serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeanzisha utaratibu wa kutoa fedha za ruzuku kwa wanafunzi wa skuli za sekondari na kuanza kutoa elimu hiyo bila malipo. Kwa upande mwengine serikali itatoa ruzuku ya ufaulu kwa skuli za msingi na sekondari zitakazoongoza kwa ufaulu katika masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiengereza. Sambamba na hayo, serikali imetenga TZS 8 bilioni na Benki ya Dunia imetenga Dola za Marekani 3 milioni kwa ajili ya kuwajengea ujuzi walimu 665 kuweza kufundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiengereza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa afya serikali itaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa mbili la wodi za wazazi na watoto katika Hospitali ya Kivunge, sambamba na kuanza ujenzi wa wodi ya wazazi, watoto na wanawake kwa hospitali ya Chake Chake ili kuimarisha hospitali hizi kuweza kufikia katika hadhi ya Hospitali za Wilaya. Ujenzi wa Nyumba na kuendelea na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali nyengine. Kwa upande mwengine, serikali tayari imetiliana saini na *BADEA*, *KUWAIT FUND* na ipo katika hatua za mwisho za kutiliana saini na *SAUDI FUND* kwa ajili ya kuanza kwa ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, hospitali ya Wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu na hospitali ya Wazazi Muembeladu. Ukarabati huo unatarajiwa kugharimu TZS 24.9 bilioni sawa na Dola za Kimarekani 11.0 milioni. Chini ya ufadhili huo, serikali pia inatarajia kuanza ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa na kufundishia madaktari ya Binguni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wa Yuan 100 milioni sawa na TZS 35 bilioni. Serikali itaendelea na ujenzi wa nyumba za madaktari na wafanyakazi katika hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani Pemba; Utengenezaji wa studio za Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) zilizopo Rahaleo; Uwekekaji wa taa za barabarani katika barabara ya Benjamin Mkapa pamoja na ujenzi wa miradi ya maji na skuli.

Mhe. Mwenyekiti, katika uimarishaji wa sekta ya maji Serikali itakamilisha visima 20 vilivyochimbwa na Ras el Khaimah na kuimarisha miundombinu na mfumo wa usambazaji maji mijini na vijijini pamoja na uwekaji wa vifaa muhimu. Mazungumzo na Serikali ya Japani juu ya mradi mpya wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi pia yanaendelea vizuri na yanatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendeleza juhudi za kuimarisha Sekta za Michezo ambayo ni muhimu katika kuimarisha afya za jamii, kutoa burudani mbali mbali kwa wananchi na sehemu ya ajira kwa vijana. Katika mwaka 2018/19 Sekta ya Michezo itaendelezwa kwa ujenzi wa viwanja vya michezo katika wilaya za Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imedhamiria kuanzisha na kuendeleza miji midogo 14 inayojitegemea kwa Unguja na Pemba. Miji hiyo ni Nungwi, Mkokotoni, Kivunge, Mahonda, Gamba, Kitogani, Dunga, Makunduchi na Chwaka kwa Unguja na Micheweni, Konde, Wete, Mkoani na Kengeja kwa Pemba. Sambamba na hilo, serikali ina azma ya kujenga makaazi mapya ya kisasa katika maeneo mbali mbali ili kuwapatia wananchi makazi bora na kuinua haiba ya mji wa Zanzibar. Maeneo yanayokusudiwa kuendelezwa ni pamoja na Kwahani; Chumbuni; Kisima Majongoo, Kisiwandui, Miembeni na Darajani; Saateni, Mikunguni, Makadara na Mwembeladu; na Chuini kwa upande wa Unguja na Vitongoji, Tumbe na Chake Chake kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka 2018/19, serikali imekusudia kuanza na ujenzi wa makaazi ya kisasa katika eneo la Kwahani kwa kuandaa upembuzi yakinifu na kuanza kwa hatua za ujenzi.

Kukuza Uwezo wa Watu:

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha uwezo wa wataalamu na mabingwa wa fani mbali mbali na kuleta ufanisi zaidi wa kazi, serikali itaongeza juhudi za kusomesha watendaji wa fani zenye upungufu ikiwemo afya, nishati, biashara, viwanda, kilimo na ufugaji. Aidha, mafunzo ya amali na ujasiriamali yataimarishwa kwa kuendelea na ujenzi wa vituo vya amali Daya na Makunduchi na kuanza ujenzi wa skuli ya ufundi ya JKU Mtoni. Hatua hizi zitaimarisha wahitimu kuweza kujiajiri wenyewe baada ya kumaliza masomo yao, badala ya kutegemea ajira serikalini ambazo ni chache.

Utawala Bora, Uimarishaji wa Taasisi na Uwekaji Mji Katika Hali ya Usalama

Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendelea na utekelezaji wa mkakati wa mabadiliko katika sekta ya sheria ambao umekusudia kuimarisha ushirikishwaji wa umma na demokrasia nchini kwa jumla. Aidha, serikali itatilia mkazo ujenzi wa majengo na ofisi za serikali kwa kuendelea na ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu Tunguu, Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango Unguja, Ofisi ya Shirika la Utangazaji Zanzibar – Pemba, lakini vile

vile nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba na jengo la Ofisi ya Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi - Unguja. Serikali itaendelea na Uimarishaji wa Nyumba za Makaazi na Mahanga kwa Vikosi vyote vya Idara Maalum za SMZ. Katika kuimarisha suala la usalama nchini serikali inakusudia kuendelea na uwekaji wa kamera na vifaa vya ulinzi katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na katika mikoa yote mengine ya Unguja na Pemba.

Ajira kwa Vijana:

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira ya upatikanaji wa ajira kwa vijana nchini, Serikali itatilia mkazo uendelezwaji wa Programu ya Ajira kwa Vijana ambayo itajikita kuwawezesha vijana wa rika mbali mbali na elimu tofauti kupata ajira katika maeneo mbali mbali yakiwemo ya kilimo hasa cha mboga, ufugaji wa kuku na samaki; eneo la viwanda ikiwemo usarifu wa matunda na mboga, useremala na ushoni; eneo la mazingira ikiwemo huduma za usafi wa Miji na Manispaa na kuwajengea uwezo kupitia fani mbali mbali za sanaa na michezo. Maelezo zaidi juu ya jitihada zinazoendelezwa na serikali nitayatoa alasiri ya leo wakati nitakapowasilisha Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/19. *(Makofi)*

Kuendeleza Tafiti:

Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendelea na juhudi za kufanya tafiti juu ya masuala ambayo yataleta tija kwa maendeleo ya taifa, ikiwemo tafiti juu ya masuala ya kilimo, mifugo, afya, nishati mbadala na mafuta na gesi asilia. Aidha, kwa kuendeleza na kuimarisha masuala ya utafiti serikali imeanzisha taasisi tatu za utafiti ambazo ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar iliyopo Kizimbani (*ZARI*), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo iliyopo Kizimbani (*ZALIRI*) na Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar iliyopo Binguni (*ZIHR*). Kutokana na umuhimu wa utekelezaji wa tafiti Wizara zote zina idara za Mipango, Sera na Utafiti zinazosimamia masuala ya utafiti katika taasisi zao na kutenga fungu maalum la utafiti fungu ambalo limetengwa katika Tume ya Mipango ya Zanzibar. Vile vile, serikali inaendelea kupata msaada wa kufanya tafiti kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (*COSTECH*) chini ya ofisi ya uratibu iliyopo hapa Zanzibar.

RASILIMALI KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2018/19

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2018/19, Mpango wa Maendeleo unalenga kutekeleza jumla ya programu 27 na miradi 55 ya maendeleo (miradi 14 mipya). Jumla ya TZS 612.95 bilioni zitatumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS 116.35 bilioni sawa na asilimia 23.43 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2017/18 ambayo ilikuwa ni TZS 496.60 bilioni.

Serikali imepanga kutumia TZS 148.75 bilioni kutokana na fedha za ndani sawa na asilimia 24.3 ya Bajeti ya Maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS 32.63 bilioni sawa na asilimia 28.1 ya Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2017/18. Kati ya fedha za serikali (TZS

148.75 bilioni), TZS 97.29 bilioni ni kwa programu na miradi ya kimkakati, yenye mikataba au dhima (*Commitment*) na TZS 51.46 bilioni kwa miradi mengine.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya TZS 464.20 bilioni sawa na asilimia 75.7 zimepangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 75.56 bilioni ni ruzuku na TZS 388.64 bilioni ni mikopo. Fedha hizo ni ongezeko la TZS 83.71 bilioni sawa na asilimia 22.0 ikilinganishwa na makisio kwa mwaka 2017/18 ya jumla ya TZS 380.5 bilioni.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia hotuba yangu hii napenda niishukuru Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae na Mhe. Bahati Khamis akiwa Makamu Mwenyekiti. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hii kwa maoni na ushauri waliyotupatia. Mawazo yao yamesaidia kuimarisha Mpango wetu wa Maendeleo ili kuwa na tija kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, aidha naomba kutoa shukurani za kipekee kwa watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji Ndugu Juma Hassan Reli kwa matayarisho ya hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kumshukuru Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Aidha, natoa shukurani kwa Makatibu Wakuu wa Wizara zote za SMZ wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika matayarisho ya hotuba hii. Ni matumaini yangu kwamba tutashirikiana zaidi katika utekelezaji wa kazi katika siku zijazo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa aina ya kipekee naomba kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa na Nchi Wahisani kwa misaada ya kifedha na kitaaluma wanaoendelea kutupatia yakiwemo Mashirika yafuatayo:

ACRA, AFYA BORA, AfDB, BADEA, CARE AUSTRIA, CHINA, CANADA, CIDA, COSTECH, DFID, EAC, EGH, EGYPT, EU, EXIM BANK CHINA, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GLOBAL FUND,GPE, INDIA, ICAP, IFAD, ILO, IMF, OPEC, JAPAN, JICA, KOREA, MILELE FOUNDATION, NMB, NORWAY, OFID, ORIO - NETHERLAND, OMAN, PMI, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, SWEDEN, UK, UNDP, UNFPA, UNICEF, URT, USAID, UN WOMEN, WB, na WHO. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee na lijadili Mwelekeo wa Uchumi kwa mwaka 2018 na kuidhinisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe Waziri wa Fedha na Mipango, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa na taarifa kidogo ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambaye katika uwasilishaji wake kuna maeneo ameyasahau kuyasoma na ni ushauri wa jumla wa kamati. Kwa hivyo, haya yote naomba yaingie kwenye *hansard*.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa kanuni zetu na mpangilio wa kazi za sasa asubuhi katika *order paper* zetu umekwisha, sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuweka kando kanuni ya muda. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa umekuwa ni utamaduni wetu kusoma Bajeti ya Serikali wakati wa saa 10 Alasiri jioni, na kwa kuwa kanuni yetu ya 23(1) ambayo inaongoza muda wa shughuli za Baraza, nikuombe Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe tuweke kanuni ya muda kando ili baada ya kuanza shughuli zetu saa 11:00 jioni leo sasa tuanze saa 10 jioni ili kuendelea na utamaduni wetu ambao umezoeleka na kutoa muda wa kutosha kwa Mhe. Waziri wa Fedha kuwasilisha Bajeti ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kuweka kando kanuni ya muda ya 23(1) ili tuanze shughuli yetu saa 10:00 jioni barabara. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Kabla ya kuakhirisha kikao chetu hiki kuna tangazo kutoka kwa Mnadhimu, Wawakilishi wote wa CCM wanatakiwa kufika katika ukumbi wa juu baada ya kuakhirishwa kikao hiki. Waheshimiwa Wajumbe nami niwashukuru kwa utulivu wenu na kwa uwasilishaji wa Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, sasa naomba niakhirishe kikao hiki hadi saa 10:00 jioni.

(Saa 5:22 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 10:00 jioni)

(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nitasoma orodha ya wageni tulionao mwisho wa shughuli yetu kwa sababu sina hapa sasa hivi hiyo orodha, lakini kwa heshima na taadhima nimesimama niwaombe *sergeant at arms,* ili waweze kwenda kututafutia na kutuletea Mhe. Waziri wa Fedha, ili aje awasilishe Bajeti Kuu ya Serikali. *Sergeant at arms* naomba mkanitafutie Waziri wa Fedha na Mipango mumlete. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango karibu sana.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, natanguliza shukrani kwa Mola wetu muumba na muweza kwa kutujaalia sote uhai, uzima na neema nyengine zilizotuwezesha kukutana tena alasiri hii ili kutimiza wajibu wetu muhimu kwa jamii tunayoitumikia na kuiongoza. Wajibu huu unatokana na matakwa ya Kifungu cha 106 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 41(3) cha Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Mhe. Spika, vifungu hivyo vinamtaka Waziri anayehusika na Fedha, kabla ya kumalizika mwaka wa Fedha, kutayarisha na kuyawasilisha Baraza la Wawakilishi Makadirio ya Bajeti ya mwaka unaofuata. Kwa kuwa mwaka wa fedha wa 2017/18 unakaribia kumalizika, Mapendekezo haya ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2018/19 yanawasilishwa ili kutimiza matakwa hayo ya Kikatiba na Sheria.

Mhe. Spika, kwa sababu hiyo na kwa heshima kubwa, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati Maalum ya kujadili Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018/19. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jamii inayorudi nyuma kwa maendeleo yake ya kiuchumi, au yenye migogoro miongoni mwake, au baina yake na serikali inayoingoza, au iliyokata tamaa kwa maisha yake ya baadae ni chachu kwa kukosekana amani ya kudumu na maendeleo ya kweli. Wakati tukielekea kukamilisha mwaka mwengine wa fedha na wa utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2015, nchi yetu imeendelea kupata mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii; imeshuhudia utulivu mkubwa na mashirikiano ya wananchi na serikali yao; na imeendelea kuleta matumaini mapya ya maisha bora zaidi kwa wananchi wake.

Mhe. Spika, kama ilivyo kwa nchi yoyote, mafanikio hayo kwa kiasi kikubwa yanatokana na serikali iliopo madarakani na imani ya watu wa nchi kwa serikali hiyo. Kwa hivyo, mafanikio tunayoyaona kwetu hayana budi kunasibishwa na kiongozi wetu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Naomba basi nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa mwaka mwengine wa uongozi thabiti, wenye hekima na subira na wa mfano. Bado tunamuombea maisha marefu na uongozi wenye uadilifu kwa kipindi chake chote cha kutuongoza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Rais ameendelea kufaidika na ushauri na usaidizi wa karibu wa Makamu wake wa Pili, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Nasi sote tulio katika dhamana mbali mbali pia tumefarijika sana na uongozi na maelekezo ya mara kwa mara ya Mhe.

Makamu wa Pili wa Rais. Nachukua fursa hii kutambua mchango mkubwa wa jasho na fikra zake katika mafanikio tunayoendelea kuyapata na tunampongeza kwa dhati kwa uongozi wake usioyumba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwangu mimi binafsi bado naendelea kupata heshima kubwa kwa imani ya Mhe. Rais kwa kuendelea kunipa heshima ya kutumikia dhamana hii adhimu ya Waziri wa Fedha na Mipango kwa nchi yetu. Kwangu mimi hii ni heshima kubwa sana na nitaendelea kuithamini, kuishukuru na kuitumikia kwa uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa pili mfululizo tunasoma mapendekezo ya Bajeti Kuu ya Taifa wakati wizara zote zikiwa zimeshawasilisha mapendekezo ya bajeti zake. Kwa mara nyengine tena tumeshuhudia mijadala ya kina katika Baraza hili kwa mapendekezo ya bajeti kutoka Wizara za Serikali. Ni dhahiri kuwa kama taasisi, Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wako Mhe. Spika limezidi kuimarika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakupongeza sana wewe, Naibu wako Mhe. Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa Baraza, Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, kwa uimara na uweledi mkubwa mnaotumia katika kuliongoza Baraza hili. Kupitia uongozi wenu, Baraza hili tukufu na nguzo muhimu kwa mustakabali wa Zanzibar linaweza kutimiza wajibu wake wa kikatiba wa kuisimamia serikali kwa niaba ya wananchi wote wa Pemba na Unguja.

Mhe. Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umahiri na kujitolea kwao katika kuwawakilisha wananchi wa majimbo yao na kwa ujumla wao wananchi wote wa Zanzibar. Sisi tuliopo katika dhamana za serikali tunathamini sana mchango mkubwa unaotolewa na wajumbe wako katika kuimarisha utendaji wa serikali na katika kukuza demokrasia na uwajibikaji nchini.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi na pongezi, naomba nianze kwa kupitia muhtasari hali ya uchumi wetu na utekelezaji wa bajeti kwa miezi tisa ya awali kwa mwaka unaoendelea wa fedha wa 2017/18.

HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO

Mhe. Spika, maelezo ya kina ya mwenendo wa uchumi na matokeo yake katika maendeleo yetu niliyatoa leo asubuhi wakati nilipowasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2017 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/18.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza asubuhi, uchumi wetu umeendelea kuonesha mwenendo mzuri na sikusudii kurejea maelezo yote niliyoyatoa asubuhi ya leo lakini niruhusu nigusie tena mambo muhimu ya uchumi wetu kwa mwaka uliopita, 2017 kama ifuatavyo:-

i. Pato letu halisi la Taifa limeongezeka kwa asilimia 7.5 mwaka jana ikilinganishwa na mwaka 2016 ambapo uchumi wetu ulikua kwa asilimia 6.8. Kasi hii ya ukuaji ni kubwa zaidi kuliko takriban nchi zote za ukanda

wa Afrika ya Mashariki na ni ukuaji mkubwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita; *(Makofi)*

ii. Kujitokeza kiwango cha mfumko wa bei cha asilimia 5.6 ambacho ni kidogo zaidi katika kipindi cha miaka minne iliyopita;

iii. Kufanikiwa kupata mzao mkubwa zaidi wa karafuu wa tani 8,543.9 ambazo hazijawahi kufikiwa tokea mwaka 1996/97 ambapo tani 11,368.3 za karafuu zilipatikana; *(Makofi)*

iv. Kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 227,256 mwaka 2016 hadi tani 304,800 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 34.1; na

v. Kuendelea kuimarika kwa Sekta ya Utalii ambapo idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 15.2 kutoka watalii 376,242 wa mwaka 2016 hadi 433,474 mwaka 2017.

Mhe. Spika, mwenendo wetu huu wa uchumi unapaswa kuendelezwa na kuimarishwa zaidi kwani ni chachu muhimu ya maendeleo yetu. Tayari tunashuhudia kuimarika kwa mapato yetu ya ndani, kama nitakavyoeleza baadae, kutokana na kuimarika kwa uchumi huo. Mafanikio haya ni matokeo ya hali njema ya amani na utulivu inayovutia uwekezaji na shughuli za biashara, sera nzuri zilizopo, na uongozi thabiti na wa uadilifu wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. *(Makofi)*

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2017 – MACHI 2018)

Makadirio ya Mapato

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 1,087.4 bilioni ikijumuisha mapato kutokana na vyanzo vya ndani jumla ya TZS 675.8 bilioni sawa na asilimia 21.8 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 627.0 bilioni zilipangwa zitokane na makusanyo ya vyanzo vya kodi. Kitaasisi, asilimia 55.4 ya mapato hayo yalitarajiwa kukusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), sawa TZS 347.3 bilioni**.**

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) Tawi la Zanzibar lilikadiriwa kukusanya TZS 258.7 bilioni sawa na asilimia 41.3 ya mapato yote ya kodi na TZS 21 bilioni, sawa na asilimia 3.3 ya mapato ya kodi yalipangwa kukusanywa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kutokana na Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa *SMT* waliopo Zanzibar. Aidha, jumla ya TZS 48.8 bilioni zilitarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbali mbali visivyo vya kodi.

Mhe. Spika, kwa upande wa misaada kutoka nje, kwa mwaka 2017/18 ilikadiriwa kupokea Ruzuku ya TZS 82.2 bilioni na Mikopo ya TZS 298.3 bilioni. Hivyo, jumla ya fedha zote zilizotarajiwa kutoka nje ni TZS 380.5 bilioni.

Mhe. Spika, ili kuziba nakisi iliyojitokeza ya Bajeti, Baraza lako tukufu liliidhinishia serikali kukopa jumla ya TZS 30.0 bilioni kutoka soko la ndani ili kukidhi upungufu huo wa bajeti.

Makadirio ya Matumizi

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali ilikadiria kutumia kiasi hicho cha TZS 1,087.4 bilioni kugharamia bajeti yake. Jumla ya TZS 590.7 bilioni ziliidhinishwa kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 496.6 bilioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, kati ya fedha hizo za maendeleo, TZS 116.1 bilioni ni kutokana na mapato ya ndani na TZS 380.5 bilioni kutokana na mapato kutoka nje**.**

Utekelezaji Halisi

Mhe. Spika, kwa kipindi cha miezi tisa (Julai,2017 hadi Machi, 2018), ukusanyaji wa mapato umekuwa wa kuridhisha. Kwa ujumla, serikali imemudu kukusanya jumla ya TZS 677.6 bilioni. Kati ya kiasi hicho, TZS 506.6 bilioni, sawa na asilimia 74.7 ya mapato yote ni mapato ya ndani, TZS 151.0 bilioni, sawa na asilimia 22.3 ya mapato yote ni mapato kutoka nje na TZS 20.0 bilioni ni mikopo ya ndani, sawa na asilimia 3 ya mapato yote.

Mhe. Spika, makusanyo halisi ya TZS 506.6 bilioni ni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya kipindi hicho kati ya TZS 515.1 bilioni. Katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita (2016/2017), mapato ya ndani yalifikia jumla ya TZS 389.8 bilioni. Utendaji huu unamaanisha ukuaji wa mapato kwa TZS 116.8 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 30. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kati ya mapato ya ndani, mapato ya kodi ni TZS 465.2 bilioni, sawa na asilimia 97 ya lengo la kukusanya TZS 478.5 bilioni. Mapato yasiyo ya kodi ni TZS 41.4 bilioni. Matokeo haya yanaashiria utendaji mzuri zaidi katika ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi kupitia wizara zetu. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 113 ya makadirio ya TZS 36.6 bilioni. Aidha, mapato hayo yamekuwa kwa asilimia 75 ikilinganishwa na ukusanyaji wa TZS 23.7 bilioni kwa miezi tisa ya awali ya mwaka uliopita.

Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mapitio, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilikusanya jumla ya TZS 190.5 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya TZS 193.2 bilioni. Kwa kiwango hicho cha utendaji, makusanyo ya *TRA* yameongezeka kwa asilimia 25 ikilinganishwa na ukusanyaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2016/2017 ambapo jumla ya TZS 152.5 bilioni zilikusanywa**.**

Mhe. Spika, kwa upande wa Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), makusanyo halisi yamefikia TZS 258.9 bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya TZS 269.5 bilioni. Hata hivyo, ikilinganishwa na TZS 197.5 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2016/17, *ZRB* imeonesha ukuaji mkubwa zaidi wa mapato wa asilimia 31.1. *(Makofi)*

Mhe. Spika, makusanyo ya kodi ya mapato kutoka kwa wafanyakazi wa *SMT* waliopo Zanzibar yalifikia TZS 15.75 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho. Kwa mikopo katika soko la ndani, serikali imekopa jumla ya TZS 20.0 bilioni kupitia Hati Fungani, sawa na asilimia 66.7 ya makadirio ya mwaka ya kukopa TZS 30.0 bilioni.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha mapitio (Julai, 2017 - Machi, 2018) serikali imepokea kutoka kwa nchi wahisani na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, jumla ya TZS 151.0

bilioni ambazo takriban ni asilimia 40 ya makadirio ya mwaka. Kati ya kiasi hicho, Ruzuku ni TZS 34.1 bilioni na Mikopo ni TZS 116.9 bilioni. Aidha, jumla ya TZS 3.2 bilioni zilipatikana kutokana na Misaada ya Kibajeti (*General Budget Support – GBS*) na TZS 2.6 bilioni kutokana na Misamaha ya Madeni (*MDRI*). Fedha zote zilizopatikana kutokana na misaada ya nje zimetumika kwa shughuli za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo badala ya matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa shughuli za serikali.

UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Spika, kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017, Baraza lako liliidhinisha marekebisho katika sheria mbali mbali kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa Mapato ya Serikali. Muhtasari wa utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo:

i. Sheria ya Mafunzo ya Amali *(Vocational Training Act)*

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Mafunzo ya Amali *(Vocational Training Act No. 8 ya 2006)* yamefanywa kwa kutoa tafsiri ya *Gross Monthly Emolument* ambayo mwajiriwa hatakatwa gharama za mafunzo pamoja na mavazi (*uniforms*) anazopatiwa na mwajiri wake kwa mwezi tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Kama ilivyotarajiwa, hatua hii haikuwa na athari yoyote katika ukusanyaji wa mapato bali imesaidia kuleta usawa katika mfumo wa kodi.

ii Sheria ya Ajira *(Employment Act)*

Mhe. Spika, marekebisho yamefanywa kwenye kifungu cha 100 (2) cha Sheria ya Ajira *(Employment Act No.11 of 2005)* kwa kuelekeza kuwa malipo yote ya mishahara kufanywa kupitia akaunti za benki za waajiriwa. Waajiri wengi tayari wameanza kulipa mishahara ya wafanyakazi wao kupitia benki. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya TZS 2.46 bilioni zimekusanywa kutokana na kodi zinazotokana na mishahara, sawa na asilimia 410 ya makadirio kwa mwaka.

iii Kanuni za Ada ya Biashara *(Trade Levy Regulations)*

Mhe. Spika, kwenye hili tayari serikali imeacha kutoza Ada ya Biashara *(Trade Levy*) kwa uingizaji wa pembejeo za viwandani na malighafi. Tunaamini kuwa utekelezaji wa hatua hii umeleta faraja kwa wazalishaji viwandani na utasaidia kuimarisha uendelezaji wa viwanda nchini.

iv Kutungwa kwa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa

Mhe. Spika, kama ilivyoahidi, serikali imetunga sheria hiyo ya Ushuru wa Bidhaa na utekelezaji wake umeanza rasmi mwezi wa Agosti mwaka 2017. Jumla ya TZS 1.2 bilioni zimekusanywa kutokana na hatua hii katika miezi tisa.

v. Kufutwa kwa Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996 na Kutungwa Sheria ya Ushuru wa Stempu

Mhe. Spika, sheria mpya ya Ushuru wa Stempu imetungwa na kuanza kutumika rasmi mwezi wa Julai, 2017. Sheria hiyo imechukua nafasi ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996 ambayo imefutwa. Jumla ya TZS 0.96 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 240 ya makadirio ya bajeti ya TZS 0.4 bilioni;

vi. Kutoza *VAT* Kwenye Huduma za Fedha

Mhe. Spika, utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi mwezi wa Julai, 2017. Jumla ya TZS 1.6 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 45 ya makadirio ya mwaka ya TZS 3.5 bilioni.

vii. Usajili wa Namba Binafsi za Magari *(Private Number Registration)*

Mhe. Spika, utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Disemba, 2017 baada ya kusainiwa kwa kanuni. Lengo la hatua hiyo linaelekea kufikiwa kwani kwa miezi tisa hiyo hakuna mwananchi yeyote aliyejitokeza kwa ajili ya usajili huo.

MATUMIZI

Jumla ya Matumizi

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa (Julai, 2017 - Machi 2018), kupitia Kamati ya Ukomo wa Matumizi, jumla ya TZS 695.0 bilioni zilikadiriwa kutumika. Kati ya matumizi hayo, TZS 461.6 bilioni ni kwa kazi za kawaida na TZS 233.4 bilioni ni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 matumizi halisi yalifikia TZS 681.6 bilioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya matumizi hayo TZS 457.1 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida na TZS 224.5 bilioni kwa kazi za maendeleo.

Matumizi ya Kazi za Kawaida

Mhe. Spika, matumizi ya kazi za kawaida kwa kipindi cha mapitio yalifikia jumla ya TZS 457.1 bilioni. Kiwango hicho cha matumizi kinaashiria kuongezeka kwa matumizi ya kawaida kwa asilimia 34.9 ikilinganishwa na matumizi ya kipindi kama hicho mwaka 2016/2017 ambapo jumla ya TZS 338.8 bilioni zilitumika. Kati ya matumizi hayo, matumizi ya mishahara yalifikia TZS 209.7 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ya mishahara ni sawa na asilimia 30.2 ya matumizi yote ya kipindi hicho na sawa na asilimia 45.8 ya matumizi yote ya kazi za kawaida. Aidha, kwa ujumla, Matumizi ya Kazi za Kawaida yanamaanisha ukuaji wa asilimia 40.3 ikilinganishwa na TZS 149.5 bilioni zilizotumika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, mwenendo mzuri wa uwezo wetu wa kuhudumia Bajeti umejionesha pia katika matumizi ya kuendeshea Serikali *(Other Charges).* Matumizi haya yameongezeka

kwa asilimia 23.8 kutoka TZS 66.5 bilioni zilizotumika katika miezi tisa ya awali ya mwaka 2016/17 hadi TZS 82.3 bilioni kwa miezi tisa ya mwaka huu. Aidha, ikilinganishwa na makadirio ya TZS 84.1 bilioni kwa kipindi hicho, kiwango hicho cha matumizi kinamaanisha kuwa serikali imemudu kutoa shilingi 98 kati ya kila shilingi mia moja zilizopangwa kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida. Haya ni mafanikio makubwa na ya kupongezwa na kupigiwa mfano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, taswira hiyo hiyo ya kuongezeka uwezo wa kuhudumia mambo yetu imejitokeza katika utoaji wa ruzuku kwa taasisi zetu. Ikilinganishwa na mwaka uliopita, fedha zilizotolewa na serikali kwa mwaka huu ni asilimia 68.7 zaidi. Kwa ujumla, TZS 71.2 bilioni zilitolewa sawa na asilimia 88 ya makadirio ya TZS 80.9 bilioni ya kipindi hichi. Katika kipindi kama hicho mwaka jana kiasi kilichotolewa kama ruzuku kwa taasisi zetu kilifikia TZS 42.2 bilioni tu.

Mhe. Spika, eneo jengine muhimu katika matumizi ya kawaida ni matumizi kwa ajili ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali. Matumizi hayo ni kwa ajili ya kulipia viinua mgongo, pencheni, ulipaji wa mishahara kwa Viongozi Wakuu na waliotajwa katika katiba, riba za mikopo ya ndani, malipo ya wazabuni pamoja na matumizi maalum ya serikali yanapojitokeza. Kwa miezi tisa ya awali ilikadiriwa kuwa tungetumia TZS 88.2 bilioni kwa huduma hizo kutoka TZS 80.6 bilioni zilizotumika katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Hata hivyo, matumizi halisi yalifikia TZS 93.9 bilioni sawa na asilimia 106 ya makadirio yakimaanisha pia ukuaji wa asilimia 16.5.

Matumizi ya kazi za Maendeleo

Mhe. Spika, katika kipindi cha mapitio, Kamati ya Ukomo wa Matumizi ilikadiria kuwa matumizi kwa kazi za maendeleo yangefikia TZS 233.4 bilioni. Matumizi halisi yamefikia TZS 224.5 bilioni sawa na asilimia 96 ya lengo. Matumizi kutokana na fedha zetu za ndani yameongezeka kwa asilimia 86 baada ya kufikia TZS 73.5 bilioni kutoka TZS 39.5 bilioni zilizotumika katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Hata hivyo, makadirio kutokana na fedha za ndani yalikuwa kutumia TZS 82.4 bilioni, hivyo utendaji huo ni sawa na asilimia 89.2 ya makadirio. Matumizi kutokana na misaada kutoka nje yalifikia ni TZS 151 bilioni, nayo yakionesha ongezeko la asilimia 224.7 kutoka TZS 46.5 bilioni za mwaka jana.

Mhe. Spika, ongezeko hilo limetokana zaidi na kukwamuka kwa Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar ambapo katika kipindi hicho, Benki ya Exim ya China inayofadhili mradi huo kwa mkopo nafuu ilitoa jumla ya dola za Marekani 35.2 milioni sawa na takriban TZS 78.9 bilioni.

Deni la Taifa

Mhe. Spika, serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa deni la taifa kwa dhamira ya kuhakikisha linaendelea kubaki katika kiwango kinachohimilika. Aidha, serikali inaendelea kuheshimu misingi mikuu *(Fiscal Responsibility Principles)* kama

ilivyotajwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya mwaka 2016.

Mhe. Spika, kwa upande wa deni, misingi hiyo inayosimamiwa na serikali ni pamoja na hii ifuatayo:

i. Kuhakikisha kuwa Deni la Taifa ni himilivu;
ii. Kuhakikisha kuwa kwa Kipindi cha Muda wa Kati, serikali inakopa kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Maendeleo na sio kugharamia Kazi za Kawaida;
iii. Kusimamia rasilimali na deni la umma kwa kutowabebesha mzigo mkubwa kizazi kijacho; na
iv. Kuwa na akiba inayotesheleza kuhudumia deni la nje.

Mhe. Spika, pamoja na kuzingatia misingi hiyo, hadi kufikia Machi, 2018 Deni la Taifa limekua na kufikia TZS 519.7 bilioni kutoka TZS 377.1 bilioni mwezi Machi, 2017 sawa na ukuaji wa asilimia 37.8. Katika kiasi hicho, deni la ndani ni TZS 158.3 bilioni na deni la nje ni TZS 361.4 bilioni.

Mhe. Spika, kuongezeka kwa deni kumechangiwa na sababu zifuatazo:

i. Kuanza tena kutolewa fedha za mkopo kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria ambapo jumla ya dola 35.2 milioni (TZS 78.9 bilioni) zimelipwa;
ii. Mkopo mpya wa Hati Fungani wa TZS 20.0 bilioni kati ya TZS 30.0 bilioni zilizoidhinishwa kukopwa ndani;
iii. Kuongezeka kwa kiwango cha malipo ya kiinua mgongo kutokana na kuimarika kwa maslahi ya wafanyakazi. Jumla ya TZS 17.7 bilioni zimelipwa kwa wastaafu 1,075 kwa mwaka 2017/2018 ukilinganisha na TZS 15.3 bilioni zilizolipwa kwa wastaafu 1,604 kwa mwaka 2016/2017; na
iv. Kwa deni la nje, athari ya mabadiliko ya kiwango cha kubadilishia fedha.

Mhe. Spika, pamoja na ongezeko hilo, thamani ya deni letu *(face value)* ni sawa na asilimia 16.8 ya Pato letu la Taifa la mwaka 2017. Kigezo cha uhimilivu wa deni ni kuwa lisipindukie asilimia 50 ya pato letu la taifa kwa thamani za sasa za deni *(Present Value).* Hivyo, kwa kiwango cha asilimia 16.8 kwa Pato la Taifa, bado tuna kiwango kidogo cha kudaiwa, deni letu linahimilika na tuna fursa zaidi ya kukopa tukihitaji, kwa ajili ya kuharakisha maendeleo yetu. Hata hivyo, bado inakusudiwa kuendelea kutumia busara *(prudence)* kwa Serikali kuingia katika madeni.

Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Spika, jumla ya mapato yaliyopokelewa kutokana na Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 yamefikia TZS bilioni 24.3 sawa na asilimia 89.0 ya lengo la kukusanya TZS 27.3 bilioni kwa kipindi hicho. Mapato hayo yamejumuisha makusanyo kutoka *ZRB* ya TZS 17.4 bilioni sawa na asilimia 89.2 ya makadirio ya TZS bilioni 19.5 na ya *TRA* ya TZS bilioni 6.9 sawa na asilimia 88.5 ya makisio ya TZS 7.8 bilioni.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, jumla ya TZS 34.90 bilioni zilikadiriwa kutumika kwa miradi iliyoorodheshwa chini ya Mfuko wa Miundombinu kwa mwaka 2017/18. Kwa kipindi cha mapitio, TZS 20.4 bilioni zimetumika sawa na asilimia 58.5 ya makisio.

MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI MWAKA 2017/18

Matarajio ya Mapato Julai – Juni 2017/2018

Mhe. Spika, utekelezaji wetu wa bajeti kwa kipindi kilichobakia cha robo mwaka unatarajiwa kuendelea kuchangiwa na sababu tofauti zikiwemo zifuatazo:

i. Shughuli za kiuchumi katika kipindi hicho;
ii. Utendaji wa *TRA*, *ZRB* na Wizara zetu katika kukusanya mapato;
iii. Utekelezaji wa miradi na upatikanaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;
iv. Mahitaji ya matumizi muhimu kama yatakavyojitokeza.

Mhe. Spika, kutokana na sababu hizo, matarajio ni kuwa tutaumaliza mwaka kwa kukusanya jumla ya TZS 881.4 bilioni, takriban sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani ni TZS 680.0 bilioni na mapato kutoka nje ni TZS 201.4 bilioni.

Mhe. Spika, kutofikiwa lengo la mapato kunatarajiwa kuchangiwa na kiwango cha upatikanaji wa misaada, ruzuku na mikopo kutoka nje. Hali ya ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vyetu vya ndani inatarajiwa kuwa nzuri ambapo jumla ya TZS 680.0 bilioni zinatarajiwa kukusanywa. Ikilinganishwa na lengo la kukusanya TZS 675.9 bilioni kwa mwaka huu wa fedha, matarajio ya utendaji ni sawa na asilimia 100.6 ya lengo hilo. Aidha, kwa utendaji huo kunajitokeza ukuaji wa mapato kwa asilimia 30.5 ikilinganishwa TZS 521 bilioni zilizokusanywa mwaka uliopita, 2016/17. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kati ya makusanyo hayo, mapato yanayotokana na kodi ni TZS 612.4 bilioni, sawa na asilimia 97.6 ya makadirio ya TZS 627.01 bilioni. Ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 478.3 bilioni ya mwaka wa fedha uliopita 2016/17, kiasi hicho cha mapato kitapelekea ukuaji wa mapato ya kodi wa asilimia 28.04 baina ya miaka hiyo miwili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kitaasisi, utendaji wa *TRA* unatarajiwa kufikia asilimia 96.3 kwa kukusanya TZS 249.2 bilioni. Ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo ilikusanya TZS 203.9 bilioni, mapato ya *TRA* yataongezeka kwa asilimia 22.2. Kwa upande wa *ZRB*, pia kunajitokeza ukusanyaji wa kuridhisha kwa kigezo cha kufikia lengo na ukuaji wa mapato. *ZRB* inatarajia kukusanya TZS 342.2 bilioni sawa na asilimia 98.5 na sawa na ukuaji wa asilimia 35.2 kutoka makusanyo ya TZS 253.5 bilioni yaliyopatikana mwaka uliopita 2016/17. Kodi ya Mapato kutoka Serikali ya Muungano inayosimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali inatarajiwa kufikia TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

Mhe. Spika, kuhusu mapato yasiyokuwa ya kodi, utekelezaji umeendelea kuonesha mwendo mzuri na wa kutia matumaini. Mapato haya yanatarajiwa kufikia TZS 68.1 bilioni na hivyo kuwa asilimia 38.5 zaidi ya lengo la kukusanya TZS 48.8 bilioni. Makusanyo hayo yanapelekea ukuaji wa asilimia 54.5 ikilinganishwa na TZS 43.8 bilioni zilizokusanywa kutoka kianzio hiki kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mhe. Spika, katika makusanyo hayo, Mapato ya Mawizara yanategemewa kufikia TZS 51.4 bilioni sawa na asilimia 122.9 ya makadirio ya mwaka ya TZS 41.84 bilioni; Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufika TZS 3.2 bilioni sawa na asilimia 106.7 ya makadirio ya mwaka ya TZS 3 bilioni na Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, ni TZS 13.5 bilioni sawa na asilimia 337.5 ya makadirio ya mwaka ya TZS 4 bilioni.

Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/18, matarajio ya mapato ya Mfuko wa Miundombinu ni TZS 33.6 bilioni sawa na asilimia 92.5 ya makadirio kwa mwaka huo. Kati ya kiasi hicho, *TRA* inatarajiwa kukusanya TZS 10.0 bilioni sawa na asilimia 74.1 ya lengo la kukusanya TZS 13.5 bilioni na *ZRB* inatarajiwa kukusanya TZS 23.6 bilioni kati ya lengo la TZS 21.3 bilioni, sawa na asilimia 110.8

Matarajio ya Matumizi (Julai - Juni, 2017/2018)

Mhe. Spika, hadi kufikia Juni, 2018 kwa ujumla, matumizi yanatarajiwa kufikia TZS 865.1 bilioni sawa na asilimia 80.0 ya bajeti ya mwaka ya TZS trilioni 1,087.4 bilioni. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kazi za kawaida yanatarajiwa kufikia TZS 559.2 bilioni wakati matumizi ya maendeleo yatafikia TZS 305.9 bilioni.

Matarajio ya Mpango wa Maendeleo 2017/18

Mhe. Spika, kati ya TZS 305.9 bilioni zinazotarajiwa kutumiwa na serikali kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu 27 na miradi 46 ya maendeleo, serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS bilioni 104.5 kutokana na mapato yake ya ndani na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS bilioni 201.4, zikihusisha ruzuku ya TZS 45.5 bilioni na mikopo ya TZS bilioni 155.9.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nilielezea dhamira ya serikali ya kusawazisha deni linalodaiwa Shirika la Umeme (*ZECO*) na shirika kama hilo la Tanzania Bara (*TANESCO*). Deni hilo ni kutokana na ununuzi wa umeme unaofanywa na *ZECO* kutoka *TANESCO* kwa ajili ya matumizi ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Nilieleza nia ya serikali ya kuhakikisha kuwa *ZECO* inalipa kwa ukamilifu ankara zake zote mpya kwa bei iliyokubalika na pande mbili ili kuzuia kurundikana zaidi kwa deni hilo. Nilieleza pia hatua ambazo serikali na *ZECO* zitachukua kumaliza kiasi kilichokuwa kimebakia.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa *ZECO* inaendelea kulipa kwa ukamilifu ankara zote na hivyo kuepuka kuingiwa deni jipya. Kwa mwaka huu tunaoumalizia, *ZECO* imelipa jumla ya TZS 18.5 bilioni na hivyo kufanya jumla ya deni lililolipwa kufikia TZS 23.8 bilioni. Kwa upande wake, serikali imelipa jumla ya TZS 2.0 bilioni na kwa hivyo kufanya jumla ya malipo kwa kipindi cha miaka miwili kufikia TZS 15.0 bilioni. Kwa mantiki hiyo, *ZECO* na serikali kwa pamoja wameshalipa TZS 38.8 bilioni na kubakisha deni la TZS 26.8 bilioni. Itakumbukwa pia, ili kulimaliza haraka deni hilo, SMZ imependekeza kwa Wizara ya Fedha na Mipango (SMT) kuilipa *TANESCO* moja kwa moja TZS 18.0 bilioni inazoidai kupitia katika Kodi ya Mapato ya Wafanyakazi wa SMT wanaofanyakazi Zanzibar ambazo hazijalipwa hapo kabla. *(Makofi)*

Kwa upande mwengine, Taasisi kadhaa za Serikali ya Muungano zinadaiwa na *ZECO* jumla ya TZS 1.7 bilioni ambapo itafanya jumla ya deni la SMT linalodaiwa kufikia 19.7 bilioni ambazo kama zitalipwa *TANESCO* itabakiza deni la TZS 7.1 bilioni tu. *(Makofi)*

Kwa nia njema ya kulimaliza deni hilo, katika mwezi wa Oktoba mwaka jana, Serikali ilipendekeza kwa Serikali ya Muungano kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kulimaliza deni hilo kupitia katika madeni ya marejesho ya kodi ambayo Zanzibar inaidai SMT.

Mhe. Spika, mapendekezo hayo yakikubaliwa na SMT yatasaidia katika maeneo kadhaa, kwanza yatasaidia kumaliza deni lote kwa mkupuo mmoja, lakini pili utasaidia kupunguza athari za kibajeti kwa SMZ, na tatu utapelekea SMZ kulipwa pesa zote inazodai hadi sasa kutokana na marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) na ushuru wa bidhaa. Tunaendelea kufuatilia ili kupata ridhaa ya SMT kwa nia ya kumaliza vyema suala la madeni hayo yanayodaiana pande mbili za Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana pia nilieleza uamuzi wa serikali wa kuanza na Ugatuzi wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa kwa maana ya Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Miji. Maeneo yaliyohusika na ugatuzi huo ni pamoja na Elimu ya Maandalizi na Msingi, Afya ya Msingi na Huduma za Ugani na nyenginezo katika Sekta ya Kilimo. Nina furaha kulijulisha Baraza hili kuwa ugatuzi huo umeanzwa kama ilivyopangwa na kwa ujumla shughuli hii inaendelea vizuri sana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka tunaokaribia kumalizia wa 2017/18, naomba sasa niwasilishe mapendekezo ya Bajeti kwa mwaka 2018/19 kama ninavyotakiwa na Katiba yetu ya mwaka 1984 kama ilivyorekebishwa.

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019

Mhe. Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Fedha Nam. 12 ya mwaka 2016 na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2018/2019, yalitanguliwa na uwasilishwaji wa Mwelekeo wa Bajeti katika Baraza la Wawakilishi mwezi wa Februari mwaka huu. Mwelekeo huo umekuwa Dira ya utayarishaji wa Bajeti hii ambayo leo ninaiwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu, mapendekezo ya Makadirio

haya ya Mapato na Matumizi ya mwaka ujao (2018/2019) ninayowasilisha leo hii yameongozwa na mwelekeo huo ulioidhinishwa bajeti na mazingatio ya vipaumbele vya taifa.

Mhe. Spika, makadirio haya ya bajeti yametokana na matarajio ya ukuaji mzuri wa uchumi kama nilivyoeleza kwa kina katika hotuba yangu leo asubuhi. Kwa ufupi, tunatarajia ukuaji mzuri zaidi wa uchumi kwa mwaka 2018 ambao utakua kwa kasi ya asilimia 7.7 itakayotokana na kukua kwa sekta za huduma, kilimo na viwanda na utakaochangiwa zaidi na ukuaji rasilimali utakaotokana na ujenzi wa miundombinu.

MWELEKEO WA MAPATO

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato ya ndani itakumbukwa kuwa wakati akizindua Baraza la Tisa la Wawakilishi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, alieleza nia ya serikali ya kuimarisha zaidi usimamizi wa mapato yetu na kuelekea zaidi kujitegemea katika kuendesha mambo yetu badala ya kutegemea Wafadhili.

Kuhusu mapato Mhe. Rais alikumbusha kuwa ahadi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa wananchi, kama ilivyobainishwa katika ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2015, ni kukusanya kiasi cha TZS 800.0 bilioni ifikapo mwaka wa 2020. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wazee wetu walishatuambia kuwa ahadi ni deni na dawa ya deni ni kulipa, na kwa deni hili kulilipa kwake ni kwa serikali hii ya CCM kukusanya angalau TZS 800.0 bilioni kutokana na vyanzo vya ndani ifikapo mwaka 2020.

Mhe. Spika, nina fahari kubwa kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa serikali imedhamiria kutimiza ahadi hiyo na hivyo kulipa deni lake kwa wananchi. Serikali inakusudia kutimiza ahadi hiyo katika mwaka ujao wa fedha 2018/19, mwaka mmoja kabla badala ya kusubiri mwaka 2020 kama ilivyoahidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mwaka 2018/19, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu yake ya saba inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, inatarajia kukusanya jumla ya TSZ 807.5 bilioni kutokana na vyanzo vya ndani. Makadirio haya ni sawa na ongezeko la asilimia 18.7 kutoka mapato ya TZS 680.0 bilioni yanayotarajiwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2017/18 kama nilivyoeleza awali.

Mhe. Spika, mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Mapato yatokanayo na kodi yanatarajiwa kufikia TZS 727.5 bilioni;
ii. Mapato ya Mawizara yanatarajiwa kuwa TZS 71.0 bilioni;
iii. Gawio la Mashirika ya Serikali ni TZS bilioni 5; na
iv. Gawio kutoka Benki Kuu (*BoT*) ni TZS 4 bilioni.

Mhe. Spika, kitaasisi mgawanyo wa jukumu la kukusanya kiasi hicho cha mapato ni kama ifuatavyo:-

i. Mamlaka ya Mapato (*TRA*) imekadiriwa kukusanya jumla ya TZS 301.1 bilioni ambapo Idara ya Forodha na Ushuru imekadiriwa kukusanya TZS 165.9 bilioni na Idara ya Kodi za Ndani TZS 135.2 bilioni;

ii. Bodi ya Mapato inatarajiwa kukusanya TZS 485.4 bilioni ikiwemo TZS 405.4 bilioni za Mapato ya kodi, TZS 71.0 bilioni Mapato ya Mawizara na TZS 9.0 bilioni za Gawio la Benki Kuu na Mashirika ya SMZ;

iii. Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inatarajiwa kusimamia upatikanaji wa TZS 21.0 bilioni zitokanazo na Kodi ya *Payee* kwa wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato ya nje, pamoja na nia yetu ya dhati ya kuharakisha kujitegemea, bado tutaendelea kushirikiana na mataifa rafiki na mashirika ya kifedha na ya Kibinaadamu ya Kimataifa katika kugharamia maendeleo yetu. Kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali inatarajia kupokea jumla ya TZS 464.2 bilioni kutokana na mikopo na ruzuku kutoka nje ya nchi. Kati ya kiasi hicho, TZS 388.6 bilioni kinatarajiwa kutokana na mikopo na TZS 75.6 bilioni ni ruzuku. Bado serikali haitaingiza moja kwa moja misaada ya kibajeti (*GBS*) katika mipango yake ya matumizi. Kwa namna hiyo tutaendelea kutumia utaratibu wa kibajeti wa *100T* ili kukidhi haja ya matumizi pindi misaada hiyo ikipokelewa kati kati ya mwaka. *(Makofi)*

MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, serikali imekuwa ikuchukua hatua maalum za kuweka utulivu wa mfumo wa kodi nchini kama njia mojawapo ya kushajihisha uwekezaji na ulipaji wa kodi kwa hiari. Kwa mara nyengine tena, serikali haipendekezi kupandisha kodi katika mwaka ujao wa fedha. Badala yake, serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Kwa mustakabali huo, hatua zinazopendekezwa ni hizi zifuatazo:-

1. **Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya mwaka 2017**

   Mhe. Spika, serikali imekuwa ikitoza ushuru wa stempu kwa bidhaa ambazo zimesamehewa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*). Miongoni mwa bidhaa hizo ni bidhaa za vyakula muhimu kwa jamii yetu kama vile mchele na unga wa ngano, bidhaa hizo zilisamehewa *VAT* kwa dhamira ya kupunguza gharama za maisha. Kwa lengo hilo hilo, serikali inapendekeza kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Stempu kwa kufuta ushuru huo kwa uingizaji, usambazaji na uuzaji wa bidhaa za mchele na unga wa ngano nchini ili kutoa unafuu zaidi kwa bei za chakula. *(Makofi)*

   Mhe. Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa katika sheria hii ni kufutwa kwa ushuru wa stempu kwenye tiketi za ndege zinazotolewa na mashirika ya kimataifa hapa Zanzibar kwa safari za nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo ni kuleta usawa wa kodi na Tanzania Bara ambayo kwa sasa

haitozi ushuru huo, hivyo kuendelea kuutoza hapa Zanzibar kunaathiri biashara hiyo.

2. **Kufanya mapitio ya mfumo wa misamaha ya ushuru wa stempu katika kuhaulisha mali *(Transfer of Property)***

   Mhe. Spika, sheria ya ushuru wa stempu inataka ushuru huo utozwe hata pale ambapo mali inahama kutoka kwa mmiliki wake kwenda kwa mtu mwengine kwa njia ya mirathi au kutoa kwa hiba bila ya kuwepo malipo kutoka kwa anayepokea. Inapendekezwa kufuta ushuru wa stempu wakati wa uhaulishaji mali *(Transfer of Property)* bila ya malipo pale mali hizo zinapohaulishwa kwa utaratibu wa urithi, na baina ya mzazi au mlezi wa kisheria, na mtoto au mume au mke wa ndoa anapompa mwenza wake kwa hiba; *(Makofi)*

3. **Kuongeza Muda wa Kuwasilisha Ritani na Malipo ya Kodi**
   Mhe. Spika, muda unaohitajika kuwasilisha ritani ya mauzo kila mwezi na muda wa kuwasilisha malipo ya kodi serikalini ni muhimu kwa walipa kodi kutimiza matakwa ya sheria na athari katika gharama za kuwajibika kisheria. Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi *(TAPA*) Nam. 7 ya mwaka 2009, kwa sasa walipa kodi wanapaswa kuwasilisha ritani kwa kodi mbali mbali si zaidi ya siku ya 10 ya mwezi unaofuatia mwezi wa mauzo. Aidha, siku ya mwisho kufanya malipo ni tarehe 15 ya mwezi huo unaofuatia mwezi wa mauzo. Baada ya mashauriano na sekta binafsi, serikali inapendekeza kubadilisha tarehe hizo na kuzichanganya kuwa siku moja kwa maana ya tarehe 20 ya mwezi unaofuatia mauzo kwa kuwasilisha ritani na kufanya malipo.

Mhe. Spika, zaidi ya hatua hizo za kisheria, serikali pia itachukua hatua za kiutawala zenye lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Miongoni mwa hatua hizo ni hizi zifuatazo:-

1. **Kutoa Muongozo wa Kodi ya Zuio *(Withholding Tax)***

   Mhe. Spika, Wizara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikizuia kodi za *VAT* na ya mapato mbali mbali wakati wa malipo kwa Wazabuni. Imebainika kuwa bado si malipo yote yanayopaswa kuzuiliwa na kuwasilishwa *ZRB* na *TRA* yanafanywa hivyo. Ili kurekebisha kasoro zilizopo kwa mwaka ujao wa fedha serikali itatayarisha na kutoa muongozo wa usimamizi na ukusanyaji wa Kodi ya Zuio *(Withholding Tax Guideline)* kwa Wizara, Idara na Taasisi mbali mbali za Serikali. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya serikali kwa TZS 8.5 bilioni;

2. **Kuimarisha Usimamizi wa Utoaji wa Leseni**

   Mhe. Spika, bado tuna tatizo la baadhi ya watu kufanya biashara bila ya kusajiliwa na *TRA* na *ZRB* na hivyo kuikosesha serikali mapato yake. Serikali itasimamia mamlaka zote za utoaji wa leseni za biashara, ikiwemo Serikali za Mitaa, kuhakikisha kuwa hakuna leseni zinazotolewa bila ya mfanyabiashara

kusajiliwa na *TRA* na *ZRB* na kuonesha hati ya kutodaiwa kodi *(Tax Clearance Certificate)* kutoka *TRA* au *ZRB.* Matarajio ni kuwa hatua hii itaiingizia serikali jumla ya TZS 4.5 bilioni;

3. **Kodi ya Majengo *(Property Tax)***

   Mhe. Spika, matayarisho ya ukusanyaji wa Kodi ya Majengo (*Property Tax*) yamefikia hatua kubwa. Serikali itaanza rasmi kutoza kodi hiyo katika mwaka ujao wa fedha (2018/19) kwa majengo ya biashara. Jumla ya TZS 5.0 bilioni zinatarajiwa kukusanywa na kuhaulishwa kwenda Serikali za Mitaa kwa kutumia vigezo maalum vya mgao vinavyokaribia kukamilishwa.

4. **Kufanya mapitio ya viwango vya Ada**

   Mhe. Spika, serikali imekuwa ikifanya mapitio ya viwango vya ada zinazotozwa katika huduma mbali mbali kwa lengo la kuvifanya viendane na mahitaji ya wakati. Serikali itaendelea na mapitio hayo katika mwaka ujao wa fedha, hatua ambayo inatarajiwa kuingiza jumla ya TZS 0.4 bilioni.

5. **Kupunguza unafuu wa Kodi ili kulinda Viwanda vya Ndani**

   Mhe. Spika, serikali imekuwa ikitoa unafuu wa ushuru wa Forodha na kodi nyengine kwa uingizaji wa bidhaa muhimu za chakula kama vile mchele, unga wa ngano na sukari. Hata hivyo, kufuatia kuimarika kwa uzalishaji nchini kupitia kiwanda cha unga wa ngano cha *Zanzibar Milling Corporation* na kufufuliwa Kiwanda cha Sukari Mahonda, inajitokeza haja ya kupunguza unafuu unaotolewa kwa uingizaji wa bidhaa hizo muhimu ili viwanda vyetu viweze kuhimili ushindani wa haki. Serikali inakusudia kupunguza unafuu unaotolewa sasa wa ushuru wa uingizaji kwa dhamira ya kuupunguza au kuuondoa kabisa. *(Makofi)*

MWELEKEO WA MATUMIZI

Mhe. Spika, serikali inakadiria kutumia jumla ya TZS 1,315.1 bilioni katika mwaka wa fedha 2018/19. Matumizi haya yanajumuisha matumizi ya kazi za kawaida ya TZS 702.2 bilioni na matumizi ya kazi za maendeleo ya TZS 613.0 bilioni. Matumizi ya kazi za kawaida yamezingatia matakwa ya misingi ya usimamizi wa fedha kama ilivyo katika kifungu cha 5(1)(b) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2016. Kifungu hiki kinaelekeza kuwa katika kipindi cha muda wa kati, matumizi ya kazi za kawaida yasipindukie mapato ya ndani.

Mhe. Spika, katika matumizi ya kawaida, jumla ya TZS 337.1 bilioni zinahitajika kwa ajili ya kulipa mishahara, posho zinazoendana na mishahara pamoja na michango ya lazima kwa ajili ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(ZSSF).* Katika mwaka huo, kiasi cha TZS 15 bilioni zimetengwa kwa ajili ya nyongeza za mwaka, upandishaji vyeo na ajira mpya. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 41.7 ya mapato ya ndani na hivyo kimezingatia matakwa ya kifungu cha 5(1)(d) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma

kinachokataza matumizi ya mishahara na maslahi kwa wafanyakazi wa umma kuwa makubwa kwa kuzingatia uwezo wa uchumi.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia mapato ya ndani yanayotarajiwa ya jumla ya TZS 807.5 bilioni, matumizi hayo kwa ajili ya mishahara yataacha salio la TZS 470.6 bilioni kwa ajili ya matumizi mengine. Aidha, kati ya jumla ya mapato hayo yanayotarajiwa kutokana na vyanzo vya ndani, yamo mapato yaliyokasimiwa matumizi maalum na hivyo kutoweza kugawanywa kwenye matumizi mengine.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2018/19, mapato hayo yenye matumizi maalum yanatarajiwa kufikia TZS 97.5 bilioni kama ifuatavyo:-

i. Fedha maalum zilizotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Miundombinu, TZS 39.4 bilioni;
ii. Asilimia 5 ya makusanyo inayobaki *ZRB* sawa na asilimia 20 sawa na TZS 20.3 bilioni;
iii. Makusanyo kwa ajili ya Mfuko wa Barabara TZS 15.8 bilioni;
iv. Ada ya Bandari kwa mchango wa madawati inatarajiwa kuwa ni TZS 1.0 bilioni;
v. Ada ya kuendeleza ujuzi *(SDL),* TZS 13.8 bilioni;
vi. Marejesho kwa Idara ya Uhamiaji Zanzibar ya TZS 6.5 bilioni sawa na asilimia 25 ya makusanyo yao; na
vii. Ada ya usalama ya uwanja wa ndege kwa ajili ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege TZS 650 milioni.

Mhe. Spika, baada ya kuondoa kiasi hicho cha TZS 97.5 bilioni zinabaki jumla ya TZS 373.1 bilioni ambazo ndio zinagaiwa kwa ajili ya matumizi ya kuendeshea serikali *(other charges),* ruzuku kwa taasisi mbali mbali na kazi za maendeleo. Ugawaji wa fedha hizo umezingatia mambo ya ziada yafuatayo:

i. Kuendeleza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015;

ii. Maeneo ya vipaumbele vya Taifa kwa mwaka 2018/19 kama nilivyovibainisha wakati nilipowasilisha Mpango wa Maendeleo leo asubuhi; na

iii. Maagizo maalum ya serikali kwa mujibu wa vipaumbele vya taifa yakiwemo ya kutoa elimu bure hadi sekondari na kuongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba kama nitakavyoeleza hapo baadae.

Mhe. Spika, zaidi ya vigezo nilivyovitaja, ugawaji wa fedha za maendeleo kwa mwaka 2018/19 umezingatia mambo ya ziada yafuatayo:-

iv. Programu na miradi ya kimkakati *(Flagship Projects)* iliyotajwa katika

MKUZA III;

v. Programu na miradi yote ambayo serikali ina dhima *(commitment)* kutoka kwa washirika wa maendeleo;
vi. Programu na miradi yote iliyokuwa haijakamilika utekelezaji wa shughuli zake kwa bajeti ya mwaka 2017/18;
vii. Miradi inayogharamiwa kupitia Mfuko wa Miundombinu.

Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi jumla ya TZS 39.4 bilioni zimekadiriwa kutumika katika kugharamia miradi maalum ya maendeleo hususan miradi ya kuimarisha miundombinu. Miradi inayotarajiwa kugharamiwa na mfuko huo kwa mwaka 2018/19 ni kama ifuatavyo:-

S/N	TAASISI	JINA LA PROGRAMU/MRADI	BAJET (Mil TZS)
1	Ofisi Ya Makamo Wa Pili Wa Rais	Ujenzi wa Nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais	850
2	Wizara Ya Biashara , Viwanda Na Masoko	Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar**	2,000
3	Wizara Ya Elimu Na Mafunzo Ya Amali	Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali (II)**	1,600
4	Wizara Ya Afya	Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu**	900
5	Wizara Ya Ardhi, Nyumba, Maji Na Nishati	(i) Usambazaji umeme vijijini**	1,000
		(ii) Kuendeleza Visima vya Ras el Khaimah	4,000
6	Wizara Ya Fedha Na Mipango	Programu ya Upatikanaji wa Rasilimali Fedha	1,000
7	Wizara Ya Ujenzi, Mawasiliano Na Usafirishaji	i)Ujenzi wa barabara ya Chake-Wete	1,000
		ii) Ununuzi wa land crafts	2,400
8	Ofisi Ya Rais Tawala Za Mikoa, Serikali Za Mitaa Na Idara Maalum Za Smz	i) Uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi	20,000
		ii) Ujenzi wa Kiwanda cha Nguo ZQTL(Ununuzi wa vifaa na Malighafi)	1,000
9	Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo (Kmkm)	i) Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi	2,200
		ii) Ujenzi wa wodi ya wazazi KMKM	1,500
		JUMLA KUBWA	**39,450**

Mhe. Spika, kwa kuzingatia jumla ya matumizi ya TZS 1,315.1 bilioni, mapato ya ndani ya TZS 807.5 bilioni na Misaada kutoka nje ya TZS 464.2 bilioni pamoja na Mfuko wa Wafadhili *(Basket Fund)* wa TZS 3.4 bilioni, kunajitokeza matumizi kuzidi mapato kwa TZS 40 bilioni. Nakisi hiyo inaombwa kuzibwa kupitia mikopo ya ndani.

MAENEO MENGINE MUHIMU YALIYOZINGATIWA

Mhe. Spika, katika mgawanyo wa rasilimali, maeneo mengine muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

Maendeleo ya Kiuchumi

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yetu makubwa katika kukuza uchumi wetu na hatimae ukuaji huo kupelekea maendeleo ya watu wetu, bado tuna kazi kubwa sana mbele yetu kufikia katika maisha bora ya wananchi ambayo Serikali ya CCM ingependa kuyaona. Tunaendelea kushuhudia sekta za kisasa zikichukua nafasi ya sekta za asili kama vile kilimo lakini bado kasi ya mageuzi hayo inahitaji kuimarishwa zaidi. Mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato letu la Taifa kwa mwaka 2017 ni asilimia 27. Pamoja na dhamira ya kukiimarisha kilimo ili kiwe cha kisasa na chenye tija, Sekta ya Viwanda na Huduma zinapaswa kuimarishwa ili zitoe mchango mkubwa zaidi katika uchumi wetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, sambamba na kuendeleza jitihada za kushajihisha uwekezaji zaidi binafsi katika uzalishaji viwandani, serikali inatarajia kuanza ujenzi wa eneo moja la viwanda *(Industrial Park)* na eneo la kuimarisha wazalishaji wadogo wadogo. Aidha, hatua maalum za kuyaimarisha maeneo ya kusarifu mazao ya kilimo ya Kizimbani (Unguja) na Pujini (Pemba) zitachukuliwa.

Mhe. Spika, nia ya serikali ni kuona maeneo hayo yanatumiwa na wananchi pale wanapohitaji kusarifu na kuongeza thamani kwenye mazao yao. Utaratibu huu unatarajiwa kuharakisha usarifu wa mazao kwa kuondoa kikwazo cha gharama kubwa za kuwekezwa katika ujenzi wa viwanda. Kila mwenye kuhitaji kusarifu mazao yake atakuwa na fursa ya kuyapeleka kwa ajili ya kusarifiwa.

Ajira

Mhe. Spika, eneo jengine linalopewa mkazo maalum na serikali ni upatikanaji wa ajira kwa vijana wetu. Sio siri kuwa nchi nyingi zinazoendelea hasa za kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Zanzibar, zina changamoto kubwa ya kushajihisha upatikanaji wa ajira kwa nguvu kazi yake, hususan vijana. Matokeo ya Utafiti wa Nguvu Kazi wa mwaka 2014 yalionesha kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira hapa Zanzibar ni asilimia 14.3 na tatizo likijitokeza zaidi kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, kwa vijana wa umri kati ya miaka 15 hadi 24, ukosefu wa ajira umepanda kutoka asilimia 17.9 mwaka 2006 hadi asilimia 27. Hata hivyo, kwa kundi la vijana wa miaka 15 hadi 35, mafanikio yamepatikana kwa kupungua ukosefu wa ajira kutoka asilimia 31.3 mwaka 2006 hadi asilimia 21.3 mwaka 2014. Pamoja na mafanikio hayo, kiwango hicho bado ni kikubwa na kinahitaji juhudi maalum za kurekebisha.

Mhe. Spika, tatizo hili linachangiwa zaidi na uchache wa nafasi za ajira zinazojitokeza kila mwaka ikilinganishwa na mahitaji kutokana na wahitimu wanaomaliza masomo katika ngazi mbali mbali. Ili kurekebisha hali hiyo, serikali itachukua jitihada mbali mbali zikiwemo hizi zifuatazo:

a) Kuendeleza juhudi za kushajihisha uwekezaji binafsi nchini;
b) Kuendelea kukuza ujuzi wa vijana wetu na kuwapatia elimu bora ili waweze kuajirika;
c) Kuimarisha mafunzo ya ujasiriamali na amali ili vijana wengi zaidi waweze kujiajiri na kuajiri wenzao;
d) Kupitia upya utaratibu wa utoaji wa vibali vya kazi ili kuimarisha udhibiti kwa kuhakikisha kuwa wanaopatiwa vibali hivyo ni wale tu wanaostahiki na kwa nafasi ambazo vijana wa Kizanzibari hawana ujuzi wa kuzifanya; na
e) Kuendelea kuajiri vijana kwa kujaza nafasi serikalini zinazojitokeza kwa wengine kustaafu au mahitaji mapya.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada hizo, kuanzia mwaka ujao wa fedha, serikali imeamua kuanzisha Programu Maalum ya Ajira kwa Vijana. Lengo la programu hiyo ni kuwasaidia vijana kuweza kujiajiri wenyewe kwa kuwapatia mitaji kwa mapendekezo yao ya miradi katika sekta tofauti. Kwa kuanzia, serikali imetenga TZS 3.0 bilioni kwa ajili ya programu hiyo. Mazungumzo yanaendelea na Benki ya Dunia kuangalia uwezekano wa kupatikana fedha zaidi kwa programu hiyo. Programu hiyo inatarajiwa pia kunufaika na matokeo ya mazungumzo yanayoendelea na nchi ya Abu Dhabi kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu ambayo imeahidi kusaidia jitihada za serikali za kuleta ajira kwa vijana kupitia Mfuko wake wa Khalifa *(Khalifa Fund).* Ahadi hiyo ni matokeo ya ziara ya kufana na kidugu ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein katika nchi za Falme za Kiarabu aliyoifanya hivi karibuni. *(Makofi)*

Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu, nchi yetu ipo katika harakati za utafutaji wa maliasili za Mafuta na Gesi. Maelezo ya kina yametolewa na Mhe. Waziri anayesimamia sekta hiyo muhimu. Miongoni mwa mambo yaliyokwishafanyika ni pamoja na haya yafuatayo:

a) Kutungwa kwa Sheria ya Mafuta na Gesi Nam. 6 ya mwaka 2016;

b) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi *(ZPRA);*

c) Kuanza kazi za utafutaji wa rasilimali hiyo kwa kutumia ndege, meli na vifaa vya nchi kavu katika Kitalu cha Pemba/Zanzibar kwa mashirikiano na Kampuni ya *Rak Gas* kutoka Ras Al Khaimah. Tayari kazi hizo zimekamilika isipokuwa utafutaji wa mafuta katika nchi kavu kwa kisiwa cha Pemba ndio unaendelea; na

d) Kutenga eneo la Mangapwani kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mafuta na Gesi na huduma nyengine muhimu.

Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa fedha jitihada hizo zitaimarishwa zaidi kwa kuendeleza kazi ya utafutaji wa mafuta katika Kitalu hicho na kutafsiri taarifa zilizokwishakusanywa. Aidha, serikali imetenga TZS 5.0 bilioni kwa ajili ya kuanza kazi ya uwekaji wa miundombinu ya msingi katika eneo la Mangapwani. Kazi hizo ni pamoja na ujenzi wa barabara, usogezaji wa huduma ya umeme na maji.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, eneo hili la kiuchumi ni jipya kwa hapa kwetu na lina mahitaji maalum ya utaalamu na uzoefu katika fani mbali mbali zinazohusiana na mambo hayo. Kwa kuzingatia uhaba mkubwa wa utaalamu, hatua ambazo serikali inachukua kujenga haraka utaalamu ni pamoja na hizi zifuatazo:

a) Kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, serikali imetoa kipaumbele katika kudhamini wataalamu wanaosomea fani mbali mbali zinazohusiana na Mafuta na Gesi;

b) Katika Mikataba ya Ubia wa Mafuta *(Petroleum Sharing Agreements - PSA),* kunatarajiwa kuwa na kiwango maalum kwa ajili ya Kampuni hizo kutoa fedha za mafunzo ya wataalamu wazalendo; na

c) Kwa mwaka 2018/19, serikali pia imetenga TZS 1.0 bilioni kwa madhumuni ya kuharakisha ujenzi wa utaalamu huo.

Miundombinu na Huduma za Jamii

Mhe. Spika, mara nyingi nimekuwa nikieleza umuhimu ambao serikali inaweka katika kuendeleza miundombinu na huduma muhimu za Elimu na Afya. Kwa mwaka ujao wa fedha, sekta hizi tatu zimetengewa jumla ya TZS 487.5 bilioni ambapo Afya ni TZS 93.3 bilioni, Elimu na mafunzo ya Amali TZS 179.6 bilioni na Ujenzi, Miundombinu na Usafirishaji TZS 214.6 bilioni.

Mhe. Spika, kuhusu Elimu, baada ya mafanikio yaliyopatikana kwa kusajili wanafunzi wengi zaidi katika Skuli za Maandalizi na Msingi baada ya serikali kufuta michango ya wazazi katika elimu ya ngazi hizo, kuanzia mwaka ujao wa fedha serikali itafuta rasmi michango katika elimu ya sekondari. Hatua hii inaendana na dhamira ya Mapinduzi yetu matukufu ya Januari, 1964 yaliyopelekea huduma ya elimu nchini kutangazwa kutolewa bila ya malipo, bila ya ubaguzi kwa watoto wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uwekezaji huu muhimu katika kukuza watoto wetu utanufaisha watoto 256,048 wa elimu ya msingi na watoto 122,163 wa elimu ya sekondari kwa takwimu za mwaka 2017. Serikali pia itaelekeza jitihada zake katika kuimarisha ubora wa elimu na matokeo ya wanafunzi. Jitihada hizi zitapata msukumo zaidi kutokana na mashirikiano na Washirika wa Maendeleo hususan Benki ya Dunia na mashirika mengine ya Kimataifa.

Mhe. Spika, eneo jengine muhimu kwa maisha ya kila mwanaadamu ni siha, inayotokana na lishe bora, upatikanaji wa maji safi na salama, kuishi katika mazingira mazuri na kwa kuzingatia tabia njema kama vile kufanya mazoezi, na upatikanaji wa huduma bora za afya. Serikali inachukua hatua mbali mbali katika kuimarisha mambo yote hayo kama zilivyoelezwa kwa kina na Waheshimiwa Mawaziri wanaosimamia sekta hizo.

Mhe. Spika, kuhusu huduma za afya, kama nilivyotangulia kusema sekta hii imetengewa jumla ya TZS 93.3 bilioni mwaka ujao wa fedha. Moja ya eneo muhimu lililopewa mazingatio maalum ni upatikanaji wa dawa za lazima na vifaa tiba. Itakumbukwa kuwa hadi kwenye mwaka 2014, tulikuwa tukitegemea sana wafadhili hasa ndugu zetu wa Denmark kupitia Shirika lao la *DANIDA* na wa Marekani kupitia Shrika la *USAID*. Serikali ilifanya uamuzi makhsusi wa kupunguza kutegemea washirika wa maendeleo kwa upatikanaji wa dawa za lazima kwa wananchi na hatua kwa hatua kuchukua yenyewe jukumu hili muhimu.

Mhe. Spika, sambamba na uamuzi huo, bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba kutokana na fedha za ndani za SMZ imeongezeka awamu kwa awamu kutoka TZS 500 milioni mwaka 2014/2015 hadi kufikia TZS 8.0 bilioni mwaka huu unaomalizika 2017/2018. Serikali kupitia Wizara ya Afya imefanya uchambuzi wa kina wa mahitaji ya dawa za lazima na vifaa tiba na kubainisha kuwa jumla ya TZS 12.7 bilioni zinahitajika kila mwaka kwa kukidhi mahitaji hayo.

Mhe. Spika, nina furaha kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, serikali imeongeza tena bajeti ya dawa na vifaa tiba na kutenga kiasi hicho cha TZS 12.7 bilioni katika Bajeti ya Wizara ya Afya ili kukidhi mahitaji ya dawa za lazima kwa wananchi katika hospitali zetu. Ni jukumu letu sote sasa kuhakikisha kuwa dawa hizo zinanunuliwa kwa wakati, zinapatikana kwa wenye mahitaji na zinatumiwa vyema na wanaopatiwa. Kinyume cha hayo, fedha nyingi zinazotumiwa na serikali zitakuwa zinapotea bila ya malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana nilieleza juu ya Mpango wa Serikali wa kuanza kutekeleza mageuzi ya Serikali za Mitaa kwa lengo la kuongeza uwajibikaji wa umma kwa wananchi na kusogeza huduma muhimu karibu yao. Nilibainisha kuwa majukumu yatakayohamishwa kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa (ugatuzi) ni pamoja na huduma za msingi za afya, elimu ya maandalizi na msingi, na huduma za ugani na usimamizi wa madiko katika Sekta ya Kilimo na Uvuvi.

Mhe. Spika, mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mageuzi hayo umeonesha matumaini mazuri na pia kubainisha kazi kubwa iliyo mbele yetu katika kuhakikisha kuwa lengo la mageuzi hayo linafikiwa. Kwa mwaka ujao wa fedha hatua zaidi zitachukuliwa katika kuimarisha mageuzi hayo kwa maeneo ya kuanzia. Hatua hizo ni pamoja na kuhamisha wafanyakazi wa maeneo hayo kutoka Serikali Kuu na kuwahamishia Serikali za Mitaa sambamba na kuhamisha gharama zao za mishahara, maposho na likizo. Serikali itaimarisha pia uratibu wa mageuzi haya na kukabiliana na changamoto zozote zitakazojitokeza.

SURA YA BAJETI

Mhe. Spika, kwa kuzingatia hali ya mapato na matumizi niliyokwisha yaeleza hapo juu, Bajeti ya mwaka 2018/19 inatarajiwa kuhusisha mapato ya jumla ya TZS 1,275.1 bilioni. Kati ya fedha hizo:

a. Mapato ya ndani ni TZS 807.5 bilioni; na
b. Ruzuku na Mikopo kutoka nje ni TZS 464.2 bilioni

c. Ruzuku ya TZS 3.4 bilioni ya Mfuko wa Wafadhili *(BF).*

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, jumla ya TZS 1,315.1 bilioni zinatarajiwa kutumika kama ifuatavyo:

i. Matumizi ya Kazi za Kawaida TZS 702.1 bilioni, na
ii. TZS 613.0 bilioni kwa Kazi za Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia mapato ya TZS 1,275.1 bilioni na matumizi ya TZS 1,315.1 bilioni, kunajitokeza nakisi ya TZS 40.0 bilioni. Inapendekezwa kuwa nakisi hiyo izibwe kwa kukopa kiasi hicho cha fedha kutoka soko la ndani.

Mhe. Spika, kwa sura hii ya Bajeti, kunajitokeza taswira ifuatayo:

i. Mapato yetu ya ndani ya TZS 807.5 bilioni yatakidhi haja ya kugharamia matumizi yetu yote ya kazi za kawaida ya jumla ya TZS 702.1 bilioni;

ii. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo utagharamiwa na vyanzo vifuatavyo vya fedha:

a) Mapato ya Ndani ya TZS 69.4 bilioni;
b) Mfuko wa Miundombinu TZS 39.4 bilioni;
c) Mikopo kutoka nje TZS 388.6 bilioni;
d) Ruzuku kutoka nje TZS 75.6 bilioni, na
e) Mikopo ya Ndani ni TZS 40.0 bilioni.

Sura kamili ya Bajeti kwa mwaka 2018/2019 inaonekana katika jadweli hapa chini.

MFUMO WA BAJETI 2018/19						
Maelezo	**Makisio 2017/18**	**Matarajio 2017/18**	**Makisio 2018/19**	**Makisio 2019/20**	**Makisio 2020/21**	**% ya Bajeti**
MAPATO						
A Mapato ya ndani	654.9	659.0	786.5	938.8	1103.0	*20.1*
B 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS)	-	-	-			-
C PAYE kwa W/Kazi wa SMT	21.0	21.0	21.0	21.0	21.0	-
C Dhamana za Hazina na Hati Fungani	30.0	30.0	40.0		40.0	*33.3*
F Msamaha wa Madeni (MDRI)	0.0	-	-			-
G Mikopo na Ruzuku	380.5	201.4	464.2	498.8	525.7	*22.0*
H Mfuko wa Wafadhili (BF)	1.0	1.0	3.4	1.5	1.0	*237.0*
Jumla ya Mapato	**1087.4**	**912.4**	**1315.1**	**1460.1**	**1690.7**	*20.9*
MATUMIZI						
Matumizi ya Kawaida	**590.8**	**559.2**	**702.1**	**758.0**	**1007.0**	*18.8*
i) Mishahara (Wizara)	294.4	278.2	293.8	336.0	561.5	*-0.2*
ii) Mishahara (Ruzuku)	29.5	29.5	43.5	44.0	47.3	*47.3*
iii) Matumizi Mengineyo (Wizara)	101.7	91.5	148.6	145.0	152.1	*46.1*
iv) Matumizi Mengineyo (Ruzuku)	65.1	60.0	83.2	91.1	95.6	*27.8*
v) Mfuko mkuu wa Serikali (CFS)	100.0	100.0	133.0	141.9	150.5	*33.0*
Matumizi ya Maendeleo	**496.6**	**305.9**	**613.0**	**702.1**	**683.7**	*23.4*
i) Mchango wa Serikali	116.1	104.5	148.8	203.3	158.0	*28.1*
ii) Mikopo na Ruzuku	380.5	201.4	464.2	498.8	525.7	*22.0*
Jumla ya matumizi	**1087.4**	**865.1**	**1315.1**	**1460.1**	**1690.7**	*20.9*

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba katika Bajeti tunayoendelea nayo, tulitoa taarifa ya kupungua kwa utegemezi wa Bajeti kwa ruzuku kutoka nje kutoka asilimia 11.1 mwaka 2016/17 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017/18. Kutokana na mchango wa Ruzuku ya TZS 75.6 bilioni katika Bajeti ya TZS 1,315.1bilioni ya mwaka 2018/19, utegemezi wa Bajeti unatarajiwa kushuka zaidi na kufikia asilimia 5.7 tu. Haya ni mafanikio mengine makubwa tunayoendelea kuyapata ambayo yanapaswa kudumishwa. *(Makofi)*

SHUKRANI

Mhe. Spika, nina deni kubwa kwa viongozi na watendaji wote walioshiriki katika uandaaji wa Makadirio haya ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2018/19. Uwasilishaji huu usingewezekana leo hii bila ya mchango mkubwa wa maelekezo, miongozo na mawazo ya watu mbali mbali, serikalini na katika sekta binafsi. Kwa ujumla wao, naomba uniruhusu niwashukuru sana wote kwa namna walivyosaidia na kufanikisha

mimi leo hii kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba kwa dhamana niliyopewa ya Uwaziri wa Fedha na Mipango. Naomba uniruhusu niwataje wachache. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza naomba nishukuru sana maelekezo na miongozo ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Dira na upeo wa kuona mbali kwa Mhe. Rais, na utayari wake wa kutuongoza bila ya kinyongo na khiana na uzoefu wake mkubwa katika uongozi wa serikali, ni faraja kubwa kwetu sote na kwangu mimi binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kauli hiyo hiyo, namshukuru sana msaidizi wake mkuu, Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi nae kwa kutusimamia na kutuelekeza bila ya kuchoka. Tunajifunza mengi kutoka kwao muda wote. Shukrani hizi pia ni kwa Baraza la Mapinduzi na Wajumbe wake wote. Utulivu tunaoupata Wizarani na msaada mkubwa wakati wa maandalizi ya makadirio haya hauwezi kwenda bila ya kutambua na kuthamini mashirikiano ya Waheshimiwa Mawaziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Manaibu Mawaziri wote. *(Makofi)*

Pili, Mhe. Spika, ni kwako wewe binafsi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu wako Mhe. Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma tunatoa shukrani nyingi sana. Tunaelewa kazi ngumu ya kuliongoza Baraza hili. Uweledi wenu umesaidia sana kuleta utulivu wa Baraza kwa kusimamia wananchi wakiwakilishwa vyema na Wawakilishi wao, Waheshimiwa Wawakilishi wakiisimamia vyema serikali na serikali ikiwajibika kwa wananchi kupitia chombo hichi adhimu. Hakika hii si kazi nyepesi lakini mnaimudu na kuitekeleza vyema. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tatu, naomba nimshukuru sana Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Baraza lako hili. Tunapata na kuthamini sana mashirikiano makubwa kutoka kwao na kutoka kwa Kamati na Mwenyekiti wake. Miongozo na michango yao siku zote inaibua fikra mpya na za kimaendeleo na tumekuwa tukiipokea na kuifanyia kazi kwa dhati kabisa. Kwa uzito huo huo, tunashukuru sana msaada na uelewa mkubwa wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC).* Tunafanya kazi na Kamati zote hizi, na nyengine zote, kwa maelewano yasiyoathiri majukumu ya kila upande. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wapishi wa chakula chetu hiki kizuri cha Makadirio ya Bajeti ni watendaji. Naomba kumshukuru kwa dhati kabisa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Makatibu Wakuu na watendaji wote walioshiriki katika maandalizi ya bajeti hii. Michango na upeo wao umesaidia sana kuyaweka sawa makadirio haya na hivyo kuwezesha kuwasilishwa Barazani leo hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika**,** pamoja na wote hao, bado kazi kubwa ya uandaaji wa makadirio haya imefanywa na watendaji wa Wizara yangu ya Fedha na Mipango wakiwemo wa Tume ya Mipango. Nathamini na kushukuru sana uongozi na msaada mkubwa wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, ndugu yangu Bwana Khamis Mussa Omar, lakini pia Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango - Bwana Juma Hassan Reli, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango - Bwana Iddi Haji Makame, Mhasibu Mkuu wa Serikali - Bi Mwanahija Almas Ali, na Kamishna wa Bajeti - Bwana Mwita Mgeni Mwita. Kupitia kwao, nawashukuru sana watendaji wote wa Wizara, Tume ya Mipango na

Taasisi zilizo chini ya Wizara, hususan kwa mnasaba wa Mapendekezo haya, Mamlaka ya Mapato *(TRA)* na Bodi ya Mapato *(ZRB). (Makofi)*

Mhe. Spika, serikali imeendelea kushirikiana na Mataifa na Mashirika mbali mbali kwa namna moja au nyengine, mashirikiano hayo yamesaidia sana katika kuharakisha maendeleo yetu. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar natoa shukrani za dhati kwa nchi za Canada, China, Cuba, Denmark, Falme za Kiarabu, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Kuwait, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uturuki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, aidha, nashukuru sana msaada na mashirikiano na mashirika ya: ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank ya China, EXIM Bank ya Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO na WSPA. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani maalum. Kwanza, kwa wananchi wote wa Jimbo la Donge. Wakati nipo hapa nikitumikia wananchi wote wa Zanzibar, sitosahau imani kubwa ya wananchi wa Donge kwangu, kwa imani na ridhaa yao ndio walinichagua kuwawakilisha katika Baraza hili tukufu. Pili, ni shukrani kwa familia yangu yote. Kutumikia wananchi mara nyengine kunamaanisha sio tu kujitolea kwa mhusika, bali pia kunahitaji ustahamilivu, ufahamu na kujitolea kwa familia nzima. Nashukuru sana, sana uelewa na ustahamilivu mkubwa wa familia yangu na kuniunga mkono muda wote. *(Makofi)*

HITIMISHO:

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali, kwa mujibu wa Katiba yetu ya mwaka 1984 na marekebisho yake, jukumu langu kama Waziri mwenye dhamana ya Fedha ni kutayarisha na kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka ujao wa Fedha. Kwa sasa mwaka huo ni mwaka 2018/19. Jukumu la kuidhinisha Makadirio hayo ya Serikali ni la Baraza lako hili la Wananchi.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo, na kwa heshima kubwa, sasa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2018/19. Serikali inapendekeza kukusanya jumla ya shilingi trilioni moja, bilioni mia moja na kumi na tano na shilingi milioni mia moja (TZS 1.3151 Trilioni) kwa mapato hayo, mapato ya ndani ni shilingi bilioni mianane na saba nukta tano (TZS 807.5 bilioni) na ruzuku na mikopo kutoka nje ni shilingi bilioni mia nne sitini na saba nukta sita (TZS 467.6 bilioni) na shilingi bilioni arubaini (TZS 40.0 bilioni) ni mikopo ya ndani.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, kwa mwaka huo wa 2018/19, nina heshima ya kuliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya shilingi trilioni moja, bilioni mia moja

kumi na tano na milioni mia moja (TZS 1.3151 Trilioni). Matumizi hayo ni shilingi bilioni mia saba na mbili nukta moja (TZS 702.1 bilioni) kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi bilioni mia sita na kumi na tatu (TZS 613.0 bilioni) kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya uwasilishaji huo mzuri sana wa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ambaye amechukua kama saa 1:20 kukamilisha uwasilishaji wa bajeti yake na ametoa hoja na hoja yenyewe imeungwa mkono. Sasa naomba Waheshimiwa nisiwahoji ili niseme kwamba hoja hii tutaanza kuichangia siku ya Jumatatu tukijaaliwa. Natoa muda huo wa kesho pamoja na kesho kutwa ili Waheshimiwa muende mkavipitie hivi vitabu halafu baada ya hapo siku ya Jumatatu tutaanza kuchangia na kwa mujibu wa Kanuni nitakupeni dakika 20, 20 ya michango kama inavyoelekeza Kanuni.

Baada ya shukrani hiyo kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Waheshimiwa Wajumbe naomba nisome wageni ambao wametufikia leo hii, wapo katika makundi tofauti nikianza na viongozi wa kwanza kabisa ni:

Viongozi

- Mama Asha Suleiman Iddi. *(Makofi)*

Ahsanteni Waheshimiwa nafikiri huo ni ushahidi tosha kwamba kazi nzuri anayoifanya humu Balozi yupo katika hali ya usalama, Waheshimiwa wamelitambua hilo.

- Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, karibu sana Baraza la Wawakilishi.

Mabalozi Wadogo Waliokuwepo Zanzibar

- Balozi wa India
- Balozi wa Msumbiji, na
- Balozi wa Oman.

Washirika wa Maendeleo

- Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la *UNICEF. You are welcome.*

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa

- Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
- Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini

Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama

- Kamanda wa Jeshi *Nyuki Brigade Zanzibar*
- Kamishna wa Polisi Zanzibar
- Naibu Mkurugenzi Mkuu Usalama wa Taifa Zanzibar
- Kamanda wa KMKM Zanzibar
- Mkuu wa JKU Zanzibar
- Kamanda wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar
- Kamanda wa Kikosi cha Valantia Zanzibar
- Kamanda wa Zimamoto na Uokozi Zanzibar
- Naibu Mkurugenzi Idara ya Uhamiaji Zanzibar

Ahsanteni karibuni sana. *(Makofi)*

Makatibu na Wakuu wa Wizara mbali mbali za SMZ

- Makatibu Wakuu
- Manaibu Makatibu Wakuu pia wapo
- Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*
- Mhasibu Mkuu wa Serikali
- Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar
- Wenyeviti wa Tume mbali mbali
- Makamishna mbali mbali
- Wakurugenzi mbali mbali
- Viongozi mbali mbali wa siasa
- Washauri wa Mhe. Rais wa Zanzibar

Viongozi wa Siasa ambao wapo ni:

- Wenyeviti wa Mikoa wa CCM Mikoa ya Unguja
- Wenyeviti wa Wilaya wa CCM
- Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Zanzibar
- Kuna wadau mbali mbali pamoja na Waandishi wa Habari.

Ahsanteni karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe baada ya tangazo hilo la wageni na kwa sababu tumetoa huo wasaa wa kwenda kupitia Bajeti mpaka siku ya Jumatatu, hatuna shughuli nyengine yoyote ambayo itaendelea hivi sasa. Naomba nichukue fursa hii sasa niakhirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 11:29 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 25/06/2018 saa 3:00 asubuhi)